


MTU KATILI KULIKO

WOTE NIMJUAYE

 Wakati mmoja Billy Paul, mwanangu, alikuwa azungumze kwenye... kuhutubia kusanyiko huko Minneapolis, Minnesota, na ninii... yeye si mhudumu, yeye ni kama baba yake, bali alisema, “Kwanza kabisa, ninaogopa.” Kwa hiyo hilo ni kama, nadhani, ninavyojisikia asubuhi ya leo, nikisimama hapa mbele ya watu hawa wa Bwana, watumishi Wake, na kufika hapa baada ya watu kama Ndugu Oral Roberts, Velmer Gardner, na watumishi wengine mashuhuri wa Bwana wamekuwa hapa wakihubiri.

² Na halafu nilikuwa tu nikiona wakati na kusikia matangazo, inanichukua kama saa sita kuhubiri, kwa hiyo ni—nisingeweza kuwa na wakati asubuhi ya leo kwa ajili ya hilo. Kwa kawaida mimi huanza mnamo saa moja na nusu usiku na kuwaachilia kama saa saba au nane usiku, kwa hiyo karibu sina wakati. Labda nitajaribu hilo kesho alasiri.

³ Kwa hiyo ni majaliwa ya kuwa hapa asubuhi ya leo. Ninahesabu hii kuwa ni heshima kubwa ambayo ndugu wamenipa kwa njia ya Bwana, kwamba ningeweza kuja hapa na kuhutubia kiamshakinywa hiki kizuri sana asubuhi ya leo. Nikiangalia huko nje, nikiona ya kwamba ninyi, bila shaka, mlikuwa na kiamshakinywa halisi, natumaini, kiroho na kimwili pia.

⁴ Na sasa tumekuwa na wakati mzuri sana katika siku tisa zilizopita hapa kupitia Bonde la Maricopa la Phoenix, na Tempe, na Mesa, na Sunnyslope, pamoja na kundi hili la wahudumu na makanisa yao. Tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa makubwa sana kwenda, kutangulia mkutano huu mkuu, kuwahutubia na kuwaambia kwamba tunatarajia mambo mengi sana kwa wingi zaidi kuliko yote tungeweza kufanya au kuwazia, kutukia katika mkutano huu.

⁵ Ndugu Williams ameniambia hivi punde kwamba mmoja wa jamaa zake aliokoka jana usiku, ambalo lingekuwa ninii... alizama sana dhambini, nasi tunaninii... Kama mtu huyo yuko hapa asubuhi ya leo, ninamshukuru Bwana kwa ajili yako, ndugu yangu, na pamoja na wote waliookoka. Na kuomba kwamba kama kuna yeyote hapa ambaye hajaokoka, kwamba wataingia moja kwa moja mstarini asubuhi ya leo na—na kuokoka.

⁶ Nikizungumza juu ya maono, nimeninii... hiyo kidogo imekuwa ndiyo... huduma yangu ambayo Bwana alinipa, kwa

sababu ya kutokuwa na elimu ya kutosha na kadhalika, labda nisingeweza kujihesabu kama kasisi, lakini kwa njia hii ninaweza kuzungumza na watu na sio . . . niseme tu yale ni juayo, kisha Yeye anathibitisha yaliyosalia, kwa hiyo basi, kama kiasi *hicho* ni sawa, Naye aseme ni sawa, basi hayo mengine ni sawa pia. Nini . . . Wanajua jinsi ya kuzungumza ambapo mimi, labda sijui.

⁷ Ninampenda Bwana kwa sababu Yeye ni mwenye rehema sana wakati sisi hatustahili kabisa, na hata hivyo Yeye ni mwenye rehema sana. Hilo limekuwa moja ya maajabu ya maisha yangu na ujuzi wangu imekuwa ni kuona wakati tulipokuwa wasiostahili sana, na hata hivyo Yeye akatutembelea kwa vyovyote vile. Nayo inapitia tu moja kwa moja juu ya kutostahili kwetu na kutupa baraka Zake kwa vyovyote vile.

⁸ Kama vile wote wanavyojua kwamba, wengi wenu mnajua labda kwamba . . . Na ndio kwanza nisikie habari za ndugu mwingine anayepitia wakati mzito wa huzuni, kama niliopitia kwa kumpoteza mama yangu, sidhani nilimpoteza, nafikiri alitangulia tu, nafikiri, pia nasikia kwamba binti ya Ndugu Rolf McPherson alikufa. Hiyo ni kweli, ndugu? Kuna mtu yeyote . . . ? Jamani, hilo liliuhuzunisha moyo wangu wakati dada fulani aliponiambia! Wala hata sikujua hilo.

⁹ Kwa kawaida, Mungu katika rehema Zake hunionyesha watu wangu kabla hawajaondoka. Baba yangu, alifia mkononi mwangu, nami nikaikabidhi nafsi yake kwa Mungu. Ndugu zangu . . . Mimi pamoja na Ndugu Shakarian, na wengi wa wanaume hapa, tulikuwa huko, ng'ambo mwaka uliopita naamini ndivyo ilivyokuwa, na huko Jamaika, Kingston, wakati asubuhi moja kwenye kiamshakinywa Roho Mtakatifu alipoingia, nami nikasema, "Sasa, Uwepo Wake upo hapa, kujua: Je, mnamwona mama huyo anayeenda *huko* ameshika *kile* mkononi mwake? Mwiteni, aje hapa kwa muda kidogo tu." Nikamwambia hali yake.

"Ninamwona kijana mwanamume akija hapa sasa, ana jambo fulani," na kile kinachomsumbua.

¹⁰ Na papo hapo, nikaangalia chini na kumwona mtu akifa, huku kijana mwanamume amesimama, ameshikwa na degedege, ama akitema damu, nami nikasema, "Mpigie simu Billy Paul mara moja." Huyu kijana mwanamume alikuwa akitema damu. "Usimwache apande juu ya Blue Mountain leo, sijui ni nini." Na halafu baadaye, tukakuta kwamba ilikuwa ni mama mkwe wangu akifa wakati uo huo, naye shemeji yangu wa kiume amesimama pale, akiwa na degedege ya kutema damu.

¹¹ Majuma machache mwanzoni mwa Agosti nilikuwa nimeingia, naye Ndugu Arganbright akaniita niende Alaska pamoja naye kwenye safari ya kuwinda na kuanzisha tawi. Vema, mimi . . . Bwana alikuwa amenionyesha ono la, sasa,

hili ni baya sana kulazimika kutaja jambo hili, natumaini halisikiki la kukufuru, lakini, juu ya safari ya kuwinda niliyokuwa ninaenda kufanya, na niliyokuwa naenda kupata, yale niliyokuwa ninaenda kupata, ni nani alikuwa anaenda kuwa pamoja nami, na kwa nini, jinsi wangekuwa wamevalia, na vivyo hivyo hasa, kungekuwako na dubu mkali mwenye ncha za fedha na urefu wa futi tisa, angekuwa ni kuro mwenye pembe urefu wa inchi arobaini na mbili.

¹² Basi wakati aliponipigia simu, nilisema, “Hilo linasikika kama ndilo, lakini hebu nimwombe Baba kwanza.” Nami nilikuwa nimelitangazia kanisa na mahali pengi, mamia ya watu walijua habari zake. Kwa hiyo kwenda Alaska, lilisikika zuri sana, bali Roho Mtakatifu akaendelea kunionya nisiende. Na kamwe usiende kinyume na uongozi wa Roho Mtakatifu.

¹³ Ndipo siku chache baadaye mtu aliyekuwa huko British Columbia, ambaye alikuwa ni mwongofu mchanga tu, alikuwa na ndugu ambaye, nilipokuwa huko kwenye majira ya kuchipua, ambaye alikuwa na kifafa maishani mwake mwote. Nasi tulikuwa tumerudi mawindoni wakati huo baada ya ibada. Daima alikuwa amemwomba Mungu kwamba ningeweza kuona ono kwa ajili ya ndugu yake, hakuwa amewahi kuwa katika mmoja wa mikutano hiyo.

¹⁴ Lakini tulipokuwa tukitoka, tulikuwa tukisumbuka na farasi, mimi na Ndugu Eddie Byskal, ambaye nafikiri yuko hapa asubuhi ya leo, tulikuwa huko nyuma, tukisumbuliwa na farasi. Ndipo ikatokea niliangalia juu upande wa pili wa mlima, nikamwona ndugu yake, na jinsi alivyoonekana, na jambo la kufanya kwa ajili ya uponyaji wake, basi nikamwendesha mbio farasi wangu, nikampanda na kuweka mkono wangu nyuma ya matandiko ya huyo kiongozi, nikasema, “Ndugu yako...” nikatoa sifa zake.

Kasema, “Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Nenda kamlete, mtume aje huku. Halafu basi umwache peke yake mpaka atakaposhikwa na moja ya vifafa hivyo.”

Akasema, “Yeye huwa na vinne ama vitano kwa siku, na amekuwa navyo maishani mwake mwote.”

¹⁵ “Mara atakaposhikwa nacho, nyakua shati lake kutoka mgongoni mwake, ukalitupe motoni, na kusema, ‘Hili nafanya katika Jina la Yesu Kristo.’ Kitamwacha.”

¹⁶ Basi akamleta ndugu yake. Naye alikuwa ndio kwanza atoke nje ya nyumba, ilimbidi kuanza siku hiyo ku—kufyeka mahali kadhaa ili wawindaji waweze kuingia, kile tunachoita, “kufyeka mburuzo.” Naye maskini mke wake aliogopa sana... Alikuwa maskini mwanamke Mpentekoste. Na huko juu kabisa kwenye Racing River, yapata maili mia tano ama mia sita kutoka kwenye ustaarabu. Basi maskini mke huyo, wakati

mvulana huyo aliposhikwa na kifafa, mara ya kwanza, kwa kawaida yeye hurukia dirishani, lakini, aliogopa, lakini mara moja akaruka akamtagaa, akalinyakua shati lake, na kulitupa kwenye jiko salamanda, na kusema, “Hili nafanya katika Jina la Yesu Kristo.” Hajapata kushikwa na kimoja tangu wakati huo. Mnaona?

¹⁷ Na kwa hiyo akaniandikia barua na kusema, “Njoo.” Vema, huko juu. . . (Kutumikia wakati, kuokoa wakati, hasa. . .) Kuna wengi wanaoketi hapa ambao wanajua, ilisemwa hapo kabla, hasa kabisa, ninalo tangazo hilo mfukoni mwangu, dubu mkali mwenye ncha za fedha na urefu wa futi tisa, mahali pale pale hasa, wakati ule ule hasa, kuro.

¹⁸ Ndipo yule kiongozi akasema, “Unamaanisha kutoka papa *hapa* (Tunaweza kuona mpaka mahali mtu yule amesimama amevaa shati lenye mirabamiraba uliyetuambia habari zake.), ati kutoka *hapa* hadi *pale* utamwua dubu mkali mwenye ncha za fedha na urefu wa futi tisa?”

Nikasema, “Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.”

Akasema, “Itawezekanaje?”

Nikasema, “Hilo si juu yangu. Hiyo ni. . . Tayari amelinena, ninatii tu yale aliyosema Yeye.”

¹⁹ Na kwa hiyo tulipokuwa tukishuka kwenda zetu, tulikuwa katika. . . tulikuwa yapata maili tatu moja kwa moja chini ya mlima, hakuna hata mti mmoja wala chochote kile, ni kuvumwani tu ya kuro, juu ya ukingo wa misitu. Tulipokuwa katika nusu maili. . . Alikuwa amebeba kichwa wakati huo, tungebadilishana, yapata, kilikuwa na uzito wa ratili mia moja na hamsini hivi. Kwa hiyo tulikuwa. . .

Akasema, “Unasema ati hizi zitakuwa za inchi arobaini na mbili kamili?”

“Kikamilifu kabisa.”

²⁰ Ndipo tulipofika ukingoni, inchi arobaini na mbili kamili. Ndipo nusu maili, akasema, “Vema, Ndugu Branham,” kasema, “sasa huyo dubu yuko kwenye umbali wa nusu maili.”

²¹ Nikasema, “Hiyo ni kweli.” Nikageuka tu, nikasema, “Ni kitu gani *kile* kilichosimama pale *pale*?” Huyo hapo, akituungalia moja kwa moja, dubu mkali mwenye ncha za fedha na urefu wa futi tisa. Na *hili* hapa tangazo la huyo kiongozi, ninalo mfukoni mwangu.

²² Nilipofika nyumbani, mama alikuwa mgonjwa. Mimi. . . Ilikuwa ni neema ya Mungu, nilikuwa na safari zingine tatu zilizopangwa pamoja na ndugu, lakini Yeye alijua nisingeweza kuzifanya. Sasa, Mama akaniambia, “Billy, ninaenda Nyumbani.”

²³ Nikasema, “La, Mama.” Nikasema, “Kama unaenda Nyumbani, Mungu kamwe hajaniambia lolote.” Ndipo basi akaendelea, mahututi zaidi na zaidi, na hatimaye, Bwana akaiita nafsi yake Nyumbani. Nami... Ili kuwaonyesha tu kile baraka halisi ya Kipentekoste inamaanisha: Alipokuwa hawezi kabisa... Nilimwongoza mama kwa Kristo, nikambatiza mimi mwenyewe. Ndipo basi alipokuwa mahututi sana hata asingeweza kuongea tena... Aliendelea tu kuzungumza juu ya utamu wa Bwana, kasema aliniona katika ono, nimesimama, mzee kwelikweli, huku nimeshikilia msalaba, nikimnyoshea mkono.

²⁴ Ndipo basi wakati alipokuwa akiondoka, dakika chache kabla hajaondoka, asingeweza kuzungumza tena, nikasema, “Mama, huwezi kuongea tena, bali kama mwanao, ninataka kukuuliza: Je, Yesu ni mtamu tu kwako sasa kama alivyokuwa wakati ulipompokea katika umbo la Roho Mtakatifu? Kama... Unakufa sasa hivi, Mama, huwezi kuishi zaidi ya dakika zingine tano. Na kama Yesu ni mtamu vivyo hivyo kwako, ingawa huwezi kuongea, pepesa macho yako ugesi sana.” Naye angepepesa macho yake, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake. Kitu kama upepo mdogo ukapitia jengoni, ndipo nafsi yake ya thamani ikapelekwa Nyumbani.

²⁵ Nilipoenda nyumbani nilimwuliza Bwana kwa nini—kwa nini hakunionyesha. Je, ilikuwa ni kwa sababu watu wangu wengine, ningekuwa mahali mbalimbali? Ndipo nikachukua Biblia, namna *hii*, nami nikasema, “Baba...” Bibi D’Amico, yeye yuko, loo, labda kwenye mkutano huu, yeye huhudhuria yote, alikuwa ndiyo kwanza anipe Biblia yenye herufi nyekundu. Siamini katika kuchukua Neno la Mungu na kulifanya ubao wa uaguzi kutoka Kwake, lakini nilikuwa nimehuzunika moyo sana, nikizichukua tu nguo zake kule chini, naye alikuwa ni mtu mzuri, nikaivuta Biblia chini, nikasema, “Mahali fulani *Hapa* ndani unaweza kunifariji,” na cha kwanza: “Hajafa, bali amelala usingizi.”

²⁶ Kwa hiyo kesho yake asubuhi, yapata saa tatu huku nimeketi chumbani nikilia, tulikuwa tukijiandaa kushuka kwenda, tuone jinsi alivyokuwa amewekwa, ono likatokea mbele yangu, nikaona umati mkubwa wa watoto wadogo walemavu wamelala pamoja, nami nilikuwa nikiimba wimbo, *Waleteni Ndani*, na kando yake... ma—mahali hapo palikuwa nyuma sana hata pakashuka namna *hii*, na ilibidi kupainua upande wa nyuma kusudi watu wa nyuma waweze kuona mbele. Na maelfu ya watu walikuwa wamesanyika.

²⁷ Nami nikamwona mwanamke mashuhuri akiingia, ingawa alikuwa amevalia mtindo wa kale, huku amevaa sketi ndefu, na vitu vidogo shingoni, na kofia kubwa iliyopinduliwa, na nywele nyingi zimesukiwa huku nyuma. Kwa hiyo nikamwona akitembea kupitia jengoni, na, kupitia mahali hapo, hili

halikuwa ni jengo, ilikuwa ni huko nje, na kulikuwa na sanduku pande zote, kama mahali waketipo watu mashuhuri. Naye alikuwa katika sanduku hili katika dakika chache, akiwainamia watu. Nami nikaingia mimbarani na nilikuwa nikitaka kuhubiri, ndipo huyo mama akageuka kuniinamishia kichwa chake, namna *hii*, wakati alipokuwa ameinamisha kichwa chake, nikainamisha changu, nilikuwa futi tano kutoka kwake, ndipo alipoinuka, ilikuwa ni Mama, mrembo, kijana.

²⁸ Mara tu, kama *hapa*, ngurumo na radi na mngurumo, ndipo Sauti ikasema, “Usihofu juu yake tena, yeye yuko kama alivyokuwa katika mwaka wa 1906.” Nikaondoka nikaangalia katika Biblia ya kale ya familia nione kilichotukia mwaka wa 1906, na huo ndio mwaka ambao alikuwa bibi-arusi wa baba yangu. Kwa hiyo leo hii yeye ni sehemu ya Bibi-arusi wa Bwana Yesu, ambaye mimi ni mshiriki Wake. Siku moja nitamwona tena.

²⁹ Nami nina hakika ya kwamba Dada na Ndugu McPherson katika msiba wao... Pia nataka kusema ya kwamba Ndugu Tommy Hicks alinipigia simu hivi punde siku chache zilizopita, nilipoingia Phoenix hapa kwa mara ya kwanza, alimpoteza ndugu yake, nadhani imetangazwa, mmoja wa ndugu zetu. Aliuawa papo hapo huko Meksiko. Na ilimbidi Ndugu Tommy kuruka kwa ndege apate kumtambua ndugu yake, ambaye alikuwa ni mtu asiyeokoka. Na maskini Tommy alikuwa akilia, moyo wake ungevunjika.

³⁰ Nami ninatumaini ya kwamba—ya kwamba kamwe hatutakuwa na tukio hilo, bali sote tuwe tayari kwenye siku hiyo kukutana na Kristo, kwa sababu ikiwa sisi—ikiwa hatuko tayari... si vigumu kwenda wakati uko tayari, lakini, loo, wakati huko tayari!

³¹ Pia kumbukeni, hizo... hiyo haikuwa tu... huoti mambo hayo, unayaona, nayo hakika ni ya kweli. Wazee watakuwa vijana Kule, milele. Hakutakuwako na uzee tena, wala dalili yoyote ya dhambi, wala dalili yoyote ya uzee. Ni himizo jinsi gani kwetu kujua kwamba kuna Nchi ng'ambo ya mtu.

³² Ningetaka sasa, kwamba tungemkaribia kwa vichwa vilivyoinamishwa na mioyo iliyoinamishwa, huku... Mimi, kwa ajili ya mchezo mdogo tu wa kuigiza, kama vile kwa kawaida nipendavyo kufanya kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, ninataka kusoma Maandiko fulani, na kabla ya kuyasoma na kuomba, ningetaka kuuliza kama kuna mtu yeyote hapa ambaye ana haja angetaka kukumbukwa, mwinulie tu Mungu mkono wako, hata haja iwe ni nini. Loo, ni—ni kusanyiko hitaji, ulimwengu mhitaji. Na tuombe.

³³ Baba yetu wa Mbinguni, tunapoingia na kutoka miongoni mwa watu, tunajua ukweli kwamba siku moja tutafanya matembezi yetu ya mwisho. Hatuna budi kukutana kwa mara

ya mwisho duniani siku moja. Na kila wakati sisi wahudumu tunapoenda mimbarani, tunashangaa kama kutakuwako na nafasi nyingine kuwatambulisha kwa kusanyiko letu, bila kujua huo wakati utakuja lini. Basi, Bwana, tunaomba, asubuhi ya leo, utuhurumie.

³⁴ Na ninapolisoma Neno Lako lililobarikiwa, ninaomba ya kwamba hiyo Mbegu itaanguka ndani ya mioyo ya watu, hata wataipokea. Na kukiwako na yeyote hapa leo, Bwana, ambaye hajaokoka, jalia waokoke leo. Jalia wafanye uamuzi huo utoshelezao kwa yote asubuhi ya leo kwa kumkubali Mwana wa Mungu kama Mwokozi wao. Wale waliochoka kwenye Njia, na wameiacha Njia, warudishe, Bwana. Na wale walio kwenye Njia, walettee furaha, na amani, na kuridhika kwa kukubali kwao kukuu, katika nyakati zilizopita, Bwana Yesu.

³⁵ Tunajua ya kwamba hawa watu wameketi hapa tangu saa moja asubuhi ya leo, wamechoka, lakini hivi utawaburudisha, Bwana, kwa manyunyuyu ya baraka kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mbinguni cha Baba yetu? Wape, Ee Mungu, kile kinachohitajika kwa ajili ya wakati huu.

³⁶ Na sasa, pamoja na kusomwa kwa Neno Lako, nikijikabidhi mwenyewe Kwako, Ee Bwana, basi jalia Roho Mtakatifu alete mambo mengi kwa wingi sana kutoka kwenye Neno.

³⁷ Unajua haja iliyoko nyuma ya kila mkono ulioinuliwa, nami nakuomba, Baba, ya kwamba Wewe utabariki haja hiyo. Wape shauku ya moyo wao. Bariki kusanyiko hili, wakati huu wa ushirika ambapo wanaume na wanawake wa matabaka yote ya maisha kutoka kote katika taifa, na nje ya taifa hili, wamekusanyika hapa mahali hapa mashuhuri panapoitwa Phoenix, iliyotokana na utupu. Jalia Roho Mtakatifu alichukue maskini Kanisa Lake asubuhi ya leo, na kufanya finiksi kutoka Kwake, aliinue leo hii kwa miujiza, na ishara, na maajabu ya Mungu aliye hai wakati wa mkutano huu.

³⁸ Kila mmoja aliyebatizwa huko nje kwenye kidimbwi hicho cha kuogelea, ama popote pale alasiri ya leo, jalia Roho Mtakatifu atembeee juu ya maji na kumshika mtu huyo wakati wakitoka, kwa kuwa tunajua hilo agizo tumepewa na Neno la Mungu ambalo haliwezi kushindwa, hotuba kuu ya Petro kwenye Siku ya Pentekoste wakati wa kuzinduliwa kwa Kanisa, yeye alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

³⁹ Bwana, ungali unaita leo, nasi tunajua Roho Mtakatifu atashuka kwenye bonde hili, na juu ya maji haya alasiri ya leo, na kuwapa watu hao shauku za mioyo yao, akiwatia muhuri katika Ufalme wa Mungu. Tujalie, Baba.

40 Bariki mkutano huu, mbariki kila mwanamume, mvulana, ama msichana, yeyote awezaye kuwa na neno la kusema, jalia lizae matunda kwa sisi wengine. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

41 Sasa, kwa dakika chache tu za wakati wenu... nami nitamwomba Ndugu Shakarian, ama baadhi yao ambao... Mimi ni mkusini, kwanza kabisa ni mwenda pole. Kwa hiyo nilikuwa... Watu wangu huniambia ya kwamba kwa namna fulani nilikuja ulimwenguni nimechelewa; sikuzote nimechelewa. Nilipokuwa nikihubiri kwenye kanisa la Muungano wa Ndugu si muda mrefu uliopita, nami nilikuwa tu nimechelewa yapata saa moja tu, mnajua hao hawachelewi kamwe, kwa hiyo mchungaji alisimama na kusema, “Enyi kusanyiko, sasa nitawajulisha kwa *marehemu* Bw. Branham.” [Katika Kiingereza, “the late” ina maana ya “marehemu”—Mfa.]

42 Nilichelewa kwenye arusi yangu, nikamfanya mke wangu kungojea karibu saa mbili, ilinibidi kumtembelea mgonjwa. Sasa, laiti ningeweza kuchelewa kwenye mazishi yangu, hilo ndilo jambo muhimu. Vema, nina furaha sana kwamba kuna Mmoja asiyechelewa, na huyo ni Mungu na Ujumbe Wake, daima yuko kwenye wakati ufaao.

43 Sasa, kesho alasiri, Bwana akipenda, nitakuwa nikiwazungumzia, nikihubiri, Bwana akipenda.

44 Sasa, kama mngetaka kusoma fungu hili, ama kuliandika kwa ajili ya asubuhi ya leo, kwa ajili ya mchezo mdogo rahisi wa kuigiza, ningewatakeni msome Luka Mtakatifu 7:36.

Basi mtu mmoja katika Mafarisayo alimwalika ale chakula kwake. Akaingia katika nyumba yake yule Farisayo, akaketi chakulani.

45 Rahisi sana, sote tunaifahamu hadithi hiyo. Sasa, ninaamini ya kwamba hapana shaka ilikuwa karibu machweo wakati tarishi alipowasili. Alikuwa amechoka, miguu yake ilikuwa imejaa mavumbi, nywele zake zilikuwa zimefunikwa na mavumbi na jasho, kwa sababu alikuwa amekimbia karibu siku nzima, alikuwa na ju—jukumu la kutekeleza, na ilimbidi kuharakisha na kulitekeleza. Kwa hiyo labda alikuwa ameenda Kapernaumu, nao wakamwambia huko Kapernaumu, “Naam, Yeye kweli alikuwa hapa siku chache zilizopita, lakini ameondoka.” Ndipo akaenda Nazareti, na kadhalika, mji baada ya mji.

46 Hatimaye, yapata alasiri sana, jua likitua, huku amechoka, miguu inauma, mchovu, hatimaye alikuwa amekutana na yule Mtu aliyekuwa akimtafuta: Yesu wa Nazareti. Loo, laiti tungalikuwa namna hiyo, kukimbia mji kwa mji, mahali mahali, mpaka hatimaye tuko katika Uwepo Wake.

47 Hapana shaka ilikuwa ni Filipino, Filipino kidogo alikuwa mlinzi wa nje, inaonekana, walikutana naye kwanza kabla hawajawaendea wale mitume wengine. Tuseme, kwa mfano Yesu ameketi mahali fulani, na huyo hapo Yohana ameegemea kifuani Mwake, Petro akiwakilisha imani, na upendo ulikuwa karibu na Yesu kuliko wote. Kwa hiyo labda Filipino alimleta huyu tarishi kwa—kwa, hebu tuseme Petro, Petro akamleta Mbele za Yesu.

48 Naye alikuwa amechoka, Yeye, amekuwa akihubiri siku nzima, na labda sauti Yake kwa namna fulani ilikuwa imepwelea, imepwelea kwa vidonda na mavumbi ya hiyo siku, ya watu wakikanyaga ardhini na mavumbi yakitokea, nguvu Zake zime mwishia, kwa kuwa hapana shaka alisimama na kuzungumza na watu kuhusu Neno la Mungu. Alikuwa akiwaangalia na kuona jinsi walivyokuwa wakiona njaa na kiu, angewaelezea jinsi Mungu alivyozileta kazi Zake zote kuu.

49 Loo, ningalipenda kuwa huko kusikiliza Hilo! Hapana shaka, ninaamini ya kwamba kila mtu hapa angetamani kuwa kule, kusikia yale aliyosema, kusikiliza Mafundisho Yake, kilichokuwa Mafundisho Yake, jinsi alivyojieleza Mwenyewe, na namna ya sauti aliyokuwa nayo, na kuutazama uso Wake na ku—kumwona akitenda kazi Zake, na kuyatambua mawazo ya watu, na kuwaambia mambo mbalimbali na magonjwa walivyokuwa nayo, na kutangaza wameponywa. Ningependa kuwa huko. Loo, jamani, ningalitaka kuona hilo.

50 Na labda alikuwa ndiyo kwanza amalize mahubiri ya . . . Mnajua, Fundisho la kwanza la Yesu, je, mlipata kujua lilikuwa ni lipi? *Huna Budi Kuzaliwa Mara Ya Pili*. Hilo lilikuwa ndilo Fundisho Lake la kwanza, *Huna budi Kuzaliwa Mara Ya Pili*.

51 Kwa hiyo huenda alirudi kwenye Mwanzo na kuanza, na kusema, “Hapo mwanzo, Mungu alisema, ‘Na iwe,’ ikawa. Naye akasema, ‘Kila kitu nilichonena na kizae kwa jinsi yake,’ nacho kikazaa.” Ndipo huenda alileta kitu kama hiki, akisema, “Vema, sasa kwa kuwa imezaa, lakini hata hivyo, unaweza kuchukua mbegu hizi na unaweza kuzichanganya pamoja, na unaweza kupata kile kinachoitwa zao chotara, la kupendeza, zuri sana, bali si la asili. Ukiiachilia, itarudi kwa jinsi yake tena.”

52 Nayo bidhaa chotara haiwezi kamwe kustahimili magumu na utendewaji ambao ya asili inaweza kustahimili. Mbona, maskini Pembendefu angemwua kwa njaa mmoja wa Hereford wako huko mbugani kwenye majira ya baridi kali, anaweza kujimudu kama kulungu. Lakini Hereford wako chotara, Brangus wako chotara, yeye angekufa huko nje, inakubidi kumdekeza.

53 Naye . . . Kama Yeye angalikuwa amesimama siku hizi, naamini angetuambia kitu kama hicho. Si kwamba tu tumechotarisha mbegu za matunda, wanyama, bali tunayo dini chotara, haina budi kudekezwa na kupapaswapapaswa,

si ya Asili. Tunajaribu kulichukua Neno la Mungu na kulizalisha katika kitu kingine, na kulizalisha kote *hapa*, nalo linakuwa kundi la watoto wachanga dhaifu ambao inatulazimu kuwadekeza, wala hawawezi kulichukua Neno halisi. Huenda alikuwa akisema kitu kama hicho.

⁵⁴ Ndipo huenda alisema, “Mnaona, kwa kweli maisha yenu ni chotara, Baba alisema, ‘Msiuguse huo mti,’ lakini Shetani akasema, ‘Haitawadhuru,’ kwa hiyo basi, maisha yako sasa yako katika hali ya uchotara. Nao uhai huo hauwezi kujirudia wenyewe, kwa saba- . . . kujizaa tena.”

⁵⁵ Kama vile, unaweza kumchukua punda na kumzalishia kwa farasi, farasi jike, naye atazaa nyumbu, lakini huyo nyumbu, huyo mama nyumbu na baba nyumbu hawawezi kuzaa mtoto wa nyumbu, inakubidi kubaki na chotara.

⁵⁶ Jambo lile lile na mahindi, ni mazuri, bali hebu someni *Reader’s Digest*, yale vitu hivi vyote chotara vinavyowafanyia watu, kansa, chochote kile, kuku chotara. Wanasema kwamba katika miaka ishirini, kama halitakomeshwa, itakuwaje? Wanawake hawawezi kuzaa watoto tena. Wanakuwa na nguvu zaidi, wanapungua, wadogo kwenye nyonga, hawawezi kuzaa mtoto.

⁵⁷ Acha vitu jinsi vilivyo! Achana na Mungu, hivyo ndivyo Neno Lake lilivyo, liache jinsi lilivyo. Usijaribu kuongeza kitu fulani Kwake ili lipatane na kanuni ya imani, liache tu jinsi Mungu alivyolisema, liamini. Hilo litamfanya Mkristo mwenye maungo makubwa, mwenye nguvu, si mtoto mchanga ambaye hana budi kudekezwa kimadhehebu, kudekezwa kila mahali, barua kutoka kanisani, dhehebu moja hadi lingine. Wakati anapoweka jina lake kwenye kile Kitabu Mbinguni, imetatuliwa milele.

⁵⁸ Huenda Yesu alisema, “Sasa, ili kurudi kwenye yale ya asili, Mungu hana budi kunena tena.” Hivyo ndivyo anavyofanya anapokuzaa upya, maisha yako ya kale yamekwisha, nawe umerudi kwenye Neno la asili la Bwana. Wewe si ninii, wewe ni chotara katika makanisa, madhehebu, lakini wakati Mungu anaponena, anapokupa amani na Roho Mtakatifu, basi umerudi katika familia asili ya Mungu tena. Haikubidi kudekezwa basi, wewe ni Mkristo shupavu anayeweza kuvumilia hilo, nenda msalabani, kwenye ile tanuru ya moto, kwenye tundu la simba, ama popote pale, kwa sababu Neno la Mungu aliye hai linawaka moyoni mwako na nafsini mwako. Hiyo ni kweli. Na wote wanaweza kurudi nyuma, wote wanaweza kukugeuka na kadhalika, lakini hilo halitakomesha hata jambo moja, hilo Neno la Mungu linaloparuzua hukaa papo hapo wakati alipoinena ile Sauti ya asili moyoni mwako, “Wewe ni Wangu!”

⁵⁹ Nadhani labda juu ya kitu kama hicho, sijui, lakini huenda alikuwa akinena. Nayo sauti Yake ilikuwa imepwelea, midomo Yake ikakauka, uso Wake ni mwekundu kutokana na miale

ya moja kwa moja ya jua la Palestina, ambalo lina joto sana. Ndipo basi, labda Filipino na Petro walingojea mpaka alipomaliza, halafu labda akasema hivi mwishowe: “Tafuteni, nanyi mtapata.”

⁶⁰ Na mnamo wakati alipomaliza hayo, huenda Petro alisema, “Bwana, huyu hapa mtu ambaye ametumwa kutoka mahali fulani na mtu fulani, naye anataka kuzungumza na Wewe.”

⁶¹ Ndipo akamwambia na kusema, “Endelea.” Hachoki mno asiweze kusikiliza chochote unachotaka kusema. Ni yeye yule leo, haidhuru kumechelewa jinsi gani usiku, jinsi anavyoweza kuwa mchovu, Yeye angali yuko tayari kujibu lolote, swali, ambalo utamwuliza.

⁶² Naye akasema, huyu tarishi labda alidhani huu ulikuwa ni . . . wakati ambapo safari yake ilikuwa imekwisha, kwa hiyo akamwambia, “Kadinali *fulani*,” askofu, nanii, “Farisayo, bwana wangu, atakuwa na karamu *kubwa*, naye amekuheshimu, kwa sababu bwana wangu ni mtu mashuhuri, naye amekuheshimu, ukiangalia umati uliokuzunguka.” Kwa maneno mengine, “Unaona jinsi ulivyovalia? Na hata hivyo anataka uje na kumtembelea kwenye karamu hii wakati *fulani-fulani*.”

⁶³ Yesu sikuzote huenda mahali alipoalikwa, haidhuru ni wapi, Yeye atakuja. Loo, alikuja kwenye tundu la simba wakati mmoja, kwenye tanuru ya moto. Ninaamini ilikuwa ni Daudi aliyesema, “Ningefanya kuzimu kitanda changu, Yeye atakuwa huko.” Atakuja kwa aliye maskini kuliko wote, kwa aliye tajiri kuliko wote, kwa aliye mtovu wa uadilifu kuliko wote, kwa katili kuliko wote, kwa aliye duni kuliko wote, atakuja popote anapoalikwa. Haidhuru hali yako na nafasi yako maishani ni ipi, Yeye bado atakuja. Hilo linamfanya Mungu kwangu mimi, mnyenyekevu. “Nitakuwa huko. Nenda ukamwambie bwana wako, nitakuwa huko kwenye tarehe *fulani-fulani*. Nitakuwa huko.”

⁶⁴ Tarishi huyo mwenye mashaka kuliko wote, angewezaje kufanya hivyo? Laiti ningalikuwa mahali pake. Akampa Bwana kisogo akaenda zake huku ameridhika kwamba amempendeza bwana wake. Mara nyingi sana tuna hatia ya jambo hilo. Tunavutiwa sana . . .

⁶⁵ Nilikuwa nikisoma katika Wazee wa *Nikea*, *Baraza la Baada ya Nikea*, ambapo Mtakatifu Agustino wa Hippo, akiketi pamoja na Mtakatifu Martin, siku moja, alipokuwa akimtembelea kwenye nyumba ya watawa, huko nje kwenye uwanja wa nyuma, bustanini, Mungu alimpa nafasi ya kumpokea Roho Mtakatifu, kama Martin alivyofanya, bali akamkataa, alivutiwa sana na ma—mafundisho ya sharti ya Rumi hata asingeweza kumpokea Roho Mtakatifu. Mara nyingi tunakuwa hivyo, tunavutiwa sana na mambo mengine. Wakati mwingine tunavutiwa sana na wakati hata tunapoletwa moja kwa moja Mbele ya Bwana Yesu, tunaondoka.

⁶⁶ Mtu fulani alinifurahisha hivi majuzi usiku jukwaani alipokuwa akizungumza kuhusu kwenda kwenye moja ya mikutano na kunywa viski yake na kuvuta bira. Hayo tu ndiyo aliyojua kuhusu mkutano, lakini nina furaha kwamba aliikubali hiyo nafasi. Mara nyingi sana hatufanyi hivyo, kuikubali nafasi.

⁶⁷ Mjumbe huyu akipeleka ujumbe, na akiwa Uweponi mwa Bwana Yesu, na hata hivyo alikuwa mpumbavu vya kutosha, kama ikinibidi kulisema, kugeuka na kwenda, na kuwazia kwamba alikuwa amefanya yote yaliyohitajika. Wakati mwingine tunaenda shuleni na kupata Ph.D. au LL.D., tunaingia katika mkutano wa Kipentekoste, na, kuwaambia ya kwamba siku za miujiza zimepita kwa sababu askofu alitutuma tukawaambie hivyo, na kuachana na ukweli wenyewe kwamba tuko Mbele za Yesu Kristo.

⁶⁸ Ni nafasi ya jinsi gani Mungu aliyomba mtu huyo! Maskini mtu huyo mwenye mashaka! Laiti ningalisimama pale, ningalianguka miguuni Pake, jambo la kwanza, kabla sijasema lolote kuhusu yale kadinali aliyotaka. Ningalisema, “Bwana Yesu, unirehemu mimi mwenye dhambi.” Hilo lingekuwa ndilo jambo la kwanza maishani mwangu, nikijua ya kwamba Yeye alikuwa Uzima, na Rasilimali pekee kwa Mungu ilikuwa ni kupitia Kwake, ningalimkubali, nimwache Yeye awe Mwokozi wangu binafsi kwanza, na kuacha ujumbe ambao kadinali alikuwa amenipa, au papa, au mtu wa wilaya, ama yeyote yule aliyekuwa amenipa huo ujumbe, ningalimtafuta Kristo kwanza.

⁶⁹ Nafikiri huo unapaswa kuwa ndio wajibu pekee wa kila mwanamume, mwanamke anayehudhuria mikutano hii, haidhuru mtu mwingine alisema nini, umeletwa Mbele za Kristo. Haidhuru umefanikiwa jinsi gani, au hujafanikiwa, haidhuru u mkuu jinsi gani, au maskini jinsi gani, haidhuru wewe ni nini, kwenye nafasi ya kwanza, anguka miguuni Pake na kusema, “Bwana, unirehemu mimi, mwenye dhambi.” Kisha uje, uwaambie wafanyabiashara ungetaka kujiunga na matabaka yao. Mtangulize Mungu.

⁷⁰ Mtu huyu mwenye mashaka sana, jinsi ambavyo tungemwanguka asubuhi ya leo kama tungeweza kufungua pazia, na kuona kama huo ndio uliokuwa msimamo wake sikuzote, kuondoka Uweponi mwa Kristo, wakati alipokuwa na nafasi ya kusimama karibu Naye. Ni mtu mwenye mashaka jinsi gani hata wa leo, kwa sababu anaishi mahali fulani. Na huenda ikawa ni mimi na wewe baada ya mkutano huu leo, inategemea mtazamo wetu wakati tukiwa Uweponi Mwake. Sikuzote ikubali.

⁷¹ Lakini alimpa Bwana kisogo akaondoka akijisikia amefarijika, ameridhika, kwamba alikuwa amefanya yale aliyambiwa afanye. Wakati mwingine si vizuri kufanya yale unayoambiwa ufanye, katika kisa hicho, ilikuwa sawa.

⁷² Kwa hiyo basi tunaona ya kwamba hapana shaka alirudi upesi na kuleta lile agizo, na, “Nilimpata. Na—najua yeye ni nani, nilikutana naye, nami nilimwambia, na nina ahadi yake kwamba atakuwa hapa. Atakuwa hapa, alisema atakuwa hapa.”

⁷³ Sasa, kuna kasoro katika mandhari hii, kuna kasoro mahali fulani. Hao Mafarisayo hawakumpenda Yesu, walimchukia. Wasingeweza kupata Jina Lake kwenye orodha yao ya madhehebu. Wasingeweza kupata shule yoyote yao ya theolojia ambayo Yeye alikuwa amepitia, bali alikuwa amepitia moja, si yao, ya Mungu. Kwa hiyo tunaona ya kwamba hawa Mafarisayo walimchukia, Yeye hakuwa na ushirikiano nao, walimdharau.

⁷⁴ Wala hamwezi kukusanyika pamoja kwa ajili ya ushirika isipokuwa mna kitu fulani shirika. Hiyo ndiyo sababu tunapenda kuja kwenye mikutano hii, tuna kitu fulani shirika: Roho Mtakatifu, upendano wa ndugu, tukishirikiana sisi kwa sisi huku Damu ya Yesu Kristo ikisafisha dhambi zetu zote. Tuna ushirika, tuna kitu shirika.

⁷⁵ Unapowaona vijana wakiwa pamoja na wazee, ukimwona msichana mdogo akirandaranda karibu na nyanya wakati wote, kuna kasoro, tofauti kubwa mno katika umri wao. Mwajua, wasichana, wenye umri wa miaka kumi na sita, wanapenda kuzibua chingamu yao na, mwajua, na mambo kama hao wengine, na kuongea juu ya marafiki wa kiume. Na—na mama wazee, wanapenda kuzungumza juu ya kushona, na kukata na kushona, na kupika, na kadhalika. Nao watoto wadogo wanapenda ku—kuchezea wanasesere, ama gololi, vizibo, ama chochote kile. Lakini unapomwona maskini msichana mdogo akirandaranda karibu na nyanya, unawazia tu nyanya ana pakiti ya peremende mahali fulani, kasoro fulani, la sivyo yeye ni kipenzi cha nyanya.

⁷⁶ Kwa hiyo Farisayo huyu hapana shaka alikuwa na, kama vile tungeiita mtaani, “kadi murwa” ya kisiri kumwalika Yesu, maana alimchukia, hapakuwepo na ushirikiano. Ninawazia tu aliwaambia hao watu wengine mashuhuri katika ujirani wake, “Mnamjua yule *anayejiita* Nabii? Watu wetu wanajua ya kwamba ni telepathia, tunajua ya kwamba yeye ni mpiga ramli, wala hakuna chochote kwake.”

⁷⁷ Mnajua, hao wote hawakufa, wengi wao wangali hai. “Tunajua ya kwamba wao... Hatumwamini, shirika le—letu tayari limemshutumumu. Kwa hiyo mnajua nini? Katika karamu hii nitakayofanya, nitaona kama ninaweza kumleta huku chini, nasi tutathibitisha kwamba sivyo alivyo. Tutathibitisha ya kwamba yeye si vile anavyosema alivyo, kwa hiyo tutamleta huku chini.” Na hiyo, nionavyo mimi, ilikuwa ndiyo kadi aliyokuwa nayo ya kisiri.

⁷⁸ Loo, hawa Mafarisayo (Kulikuwa na matabaka mawili tu ya watu wakati huo, matajiri na maskini.), kwa hiyo wa—

wangeweza kufanya karamu kwelikweli. Loo, jamani, jinsi wangeweza kuifanya! Wangechukua, wangechagua wakati ufaao zaidi wa mwaka, labda wakati zabibu zilikuwa zimeiva kwelikweli katika bustani za mizabibu, na yasmini inayochanua usiku, na maua ya machungwa ya—yaliyoijaza hewa, na kulifanya tu bonde lijae harufu nzuri ya—ya hiyo harufu. Ndipo wangechukua na kumchoma mwana-kondoo. Loo, chakula kitamu! Kumchoma mwana-kondoo huyo, na—nao maskini wangesikia harufu yake huko chini mjini, vinywa vyao vingedondosha mate, lakini, kunusa harufu ya mwana-kondoo huyo akichomwa.

⁷⁹ Lakini ungeweza tu kuja kwa mwaliko. Walikuwa wamewekea uzio viwanja vyao na kadhalika, na labda wakaingia kwenye ukumbi mkubwa huko nyuma. Basi ulikuwa ni wakati halisi uliochaguliwa kwa ajili ya kile *walichokiita* ushirika wao ambao hawa makuhani na watawala walikuwa nao pamoja. Nao waliwaalika tu watu mashuhuri, kwa hiyo mnaona, Yesu angekuwa hafai kuwa pale. Mtu awaye yote aliyejazwa na Roho angekuwa hafai kuwa pale, kwa hiyo wa—walikuwa na mijadala yao yote juu ya mambo mengine.

⁸⁰ Na hilo ni jambo moja ninalopenda kuhusu mkutano wa Wafanyabiashara, si wafanyabiashara tu (Lakini ninii, mahali wanapoketi na kuzungumza juu ya vile wanavyoweza kupata kidogo upande *huyu*, na kukata kidogo kutoka kwa *huyu*, na kumnyang'anya Petro wapate kumlipa Paulo, wanasema, mwajua, na mambo kama hayo...), ninapenda mahali mnapokuja na kuzungumza juu ya Yesu, na juu ya Mungu, na juu ya Roho Mtakatifu, na kuhusu nguvu, na ufufuo, na Kuja kwa Bwana, hilo ndilo ninalopenda katika Wafanyabiashara.

⁸¹ Lakini jamaa huyu, alikuwa na tabia tofauti. Naye alikuwa, aliweka kila kitu tayari, waliochaguliwa, na bila shaka akatuma habari kote kwa makuhani wakuu wote, na maaskofu, na kadhalika, “Sasa, yeye anashuka, awe hapa. Sasa, bila shaka tutathibitisha tu kwa mara ya mwisho kwamba jamaa huyu hana chochote. Nanyi nyote shukeni mje, hamjawahi kumwona. Nasi tutatarajia labda kitu fulani ambacho tunaweza kumshikia.”

⁸² Kwa hiyo, hatimaye, kila kitu kiliwekwa katika utaratibu, siku yenyewe ikawadia kwa ajili ya hi—hiyo karamu, na ninii. . . asubuhi hiyo kila kitu kiliwekwa katika utaratibu na kila kitu tayari. Na loo, jinsi wangeweza kuitayarisha, kila kitu *kiliwekwa sawa kabisa*.

⁸³ Asubuhi hiyo, mapema sana, watumishi wote walikuwa wameamka wameshika taulo mikononi mwao ambao walikuwa wanaenda kuhudumu. Mnyama tayari alikuwa amechinjwa na kufanyiwa ikari kwenye uga wa mbele. Nazo divai zote zilikuwa zimewekwa kwenye viriba na madumu maalum, bilauri zilikuwa

zimetapakaa mezani. Nao watumishi wote walikuwa tayari kuuhudumia umati uliokuja.

⁸⁴ Usafiri ulikuwa ni kitu cha kipekee sana, walikuwa na njia tatu za usafiri: jeshi lilikuja katika magari ya farasi, tajiri akaja juu ya nyumbu, maskini akatembea. Kwa hiyo walikuwa na watu mbalimbali huko nje kuwashughulikia wageni wanapokuja, kweli ilikuwa imeandaliwa vizuri sana. Sasa, hebu na tuweke akili zetu karibu.

⁸⁵ Na kama tunavyoona, huyo labda ndiye yule mtu aliyekuwa ashughulikie magari ya farasi ya askari waliokuja, wa—walikuwa na mahali pa kushughulikia, uh, kuwafungua farasi wao na kuwaweka zizini na kuwapa chakula, na pale pa matajiri kumchukua maskini punda wao na kumweka sawa. Na—na halafu walikuwa na jamaa mwingine pale, aliiitwa mtawadha miguu, alikuwa ni mtumishi, mtu aliye na mshahara mdogo kuliko kundi lote, mtumishi, mtawadha miguu, kazi duni kuliko zote.

⁸⁶ Na wakati mwingine tunapowazia ya kwamba sisi ni *mtu mkubwa*, na huku Mtukufu mkuu sana wa Mbinguni alifanyika mwili katika Mtumishi mtawadha miguu, wakati Yeye alipokuja kuitawadha miguu ya mwanadamu! Alipokuja duniani hakuja kuwa *Mtu mkubwa*. Mungu sikuzote huwachukua wa—watu duni kufanya *mtu mkubwa* kutoka kwao. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, wanajaribu kuwa *mtu mkubwa*. Unataka kuwa mtu duni, Mungu huchukua kitu kisicho na maana, kufanyiza kitu kutokana nacho, basi inathibitisha kwamba Yeye ni Mungu.

⁸⁷ Jinsi ambavyo kazi hii duni, kutawadha miguu ya watu, naye Yesu alichukua kazi hiyo, iliyo duni kuliko zote iliyokuwako duniani, apate kuwa m—mfano. Haikumbidi kufanya hivyo, angeweza kuingia katika kinywa cha samaki na kutoa sarafu, ama—ama kunena na milima nayo ingemwaga dhahabu kwa mabilioni ya tani. Angeweza kuvuta maji kutoka kwenye kisima na kuyageza kuwa divai iliyo tamu kuliko zote nchini, angeweza kuchukua biskuti tano na samaki wawili, akawalisha watu elfu tano.

⁸⁸ Haikumbidi kufanya hivyo, bali alikuja kama mfano, jinsi Wapentekoste wanavyopaswa kuwa, kweli, akachukua kazi iliyo duni kuliko zote. Loo, hakika, hilo ndilo. . . Lakini tunajaribu kuchukua iliyo kubwa kuliko zote. Kama hatuwezi kuwa askofu, daktari, rai-. . .loo, kitu fulani, mahali pa juu sana, mambo makuu kuliko yote! Loo, jamani, tunanini tu, tumejaa mambo makubwa.

⁸⁹ Siji, ninapoalikwa namna hii, kuwapapasa na kuwabembeleza watu, Ninaomba, nasema, “Mungu, hao ni watu Wako, niseme nini ninapona hivyo vitu vikinyemelea?” Ndipo Roho Mtakatifu anaanza kuniambia, “Likemee *hili*.”

Mnaona, tunataka kitu *kikubwa*, naye Mungu huchukua kitu kidogo.

⁹⁰ Eliya alisikia upepo wenye nguvu ukienda kasi, ngurumo, radi, na tetemeko la ardhi, na kamwe havikumsumbua, bali kilichomvutia ni Sauti ndogo tulivu. Hiyo ilimfanya nabii kuweka kitu fulani juu ya uso wake akaenda kamsikiliza Mungu. Sijui kama sisi Wapentekoste hatujategemea sana upepo unaovuma, kelele nyingi, badala ya kukumbuka, ama, kusikia Sauti hiyo ndogo tulivu. Tunasikia mtetemo mwingi sana, hatuwezi kuchukua muda kuisikia ile Sauti ndogo tulivu.

⁹¹ Mwajua, mkokoteni huenda nje kondeni, unapita juu ya matuta ya barabarani na *kuru-kuru*, *kuru-kuru*, *kuru-kuru*, ukifanya kelele za kila namna, ukialika, na kulalama, na kurukaruka, lakini unaporudi umejaa vitu vizuri, unapitia kwenye matuta yayo wala haupigi kelele. Tunapaswa kupakiwa. Maadamu kuna uovu miongoni mwetu, maadamu kuna tofauti miongoni mwetu, bado hatujapakiwa.

⁹² Hebu chukua gugu, lenye kichwa chepesi, ngano inachipuka, inajishikilia juu hewani, na kutikiswa na upepo, inainua kichwa chake moja kwa moja juu, lakini inapojaa kabisa kichwani, inainama.

⁹³ Nafikiri hiyo ndiyo shida yetu sote siku hizi, makanisa. Hatujihusishi vya kutosha katika unyenyekevu halisi, si wa uongo, bali kitu ambacho unakaa hapo mpaka jambo fulani limekupata. Unyenyekevu, upepo mwingi mno na ngurumo, pasipo na sauti ndogo tulivu za kutosha, nafikiri hiyo ni kweli. Tunaangalia na kuona ya kwamba ni—ni kweli kwa sababu ya matunda linayozaa juu ya watu wetu, kwa namna fulani si kama lilivyokuwa.

⁹⁴ Turudi kwenye hadithi yetu; tatalipata hilo Jumapili. Angalieni, tunaona Mafarisayo hawa...Farisayo huyu akitayarisha kila kitu kwa ajili ya tamasha yake kubwa, kama vile tungeiita, tamasha kubwa atakayofanya. Nami ninamwangalia yu—yule mtu huko nje akiwa tayari kuyachukua magari ya farasi ya askari, na yule anayemchukua punda wa tajiri.

⁹⁵ Na—na huko Palestina, wanavaa va—vazi la nje, ambalo ni joho. Kwa ndani, wanavaa vazi la ndani linalofika magotini. Na waliposafiri siku hizo, walitembea juu ya milima na—na kuvuka, wakipitia njia za mkato, basi walipofanya hivyo, wao, wenye kutembea kwa miguu na wale waliokuwa na wanyama wa mizigo, walitembelea njia ile ile.

⁹⁶ Nao wale wanyama barabarani mahali walipotembelea, na—na kisha wakilala chini, mavumbi yalianza kulundikana, na ambapo wanyama walikuwa wamepitia nchini, kulikuwako na uvundo mavumbini. Na wakati watu wakitembea, huku vazi hili kubwa likicheza likasababisha upepo, nalo likaokota

mavumbi, nayo yakaingia kwenye maungo yao, usoni mwao, nao hawakufaa kukaribishwa kama walikuwa wakinuka namna hiyo.

⁹⁷ Kwa hiyo walikuwa na m—mtumishi mtawadha miguu ambaye angekutana na wageni mlangoni. Basi mtu yeyote alipokuja na kadi yake ya mwaliko, alikuwa na rafu nzima ya kile tungeita, kitu kama, viatu vya chumba cha kulala, vilivyotengenezwa kwa nguo ama—ama namna fulani ya vitambaa. Nazo ndara za siku hizo wakati mwingine zilikuwa ni kipande cha ubao, kama tulizo nazo, zinazoitwa ndara za Kirumi, zenye kipande cha ngozi ambapo kidole cha mguu kilingizwa katikati huku m—mguu basi ukiachwa wazi kwa ma—mavumbi.

⁹⁸ Nao walipokuwa wakitembea, wangefika mahali hapa, watoe ninii yao...kuitikia mwaliko wao. Nao wangeinama chini, wavue ndara hizi na kuziweka mahali fulani, zimeandikwa jina lao, na kunyosha mkono kwenye maungio ya meko na kuchukua jozi nyingine ya ndara laini na kuivaa miguuni mwao, ambao walikuwa tayari basi kuingia. Loo, mazulia yao, wakati mwingine, yalikuwa mazito na makubwa sana, yalikuwa...walikuwa na anasa nzuri nyumbani mwao, watu hao walikuwa matajiri.

⁹⁹ Halafu jambo lingine alilofanya mtu huyu, alitawadhwa, miguu yake, basi jambo lililofuata, alijongea kwa mgeni wa pili, naye alikuwa amesimama na taulo mkononi mwake, na chupa ndogo mkononi mwake, ndipo a—angemimina mafuta mkononi mwake, amwache ayasugulie nyuma ya masikio yake na shingoni mwake, kwa sababu uso wake ulikuwa unawaka moto, alikuwa mchafu. Naye angechukua taulo hii na kuupangusa uso wake vizuri, na—naye alikuwa sawa, uvundo ulikuwa umemtoka, ndipo akapakwa manukato, na hayo yalikuwa ya bei kubwa, ghali mno.

¹⁰⁰ Wanayapata, wananiambia, kutoka huko juu sana milimani ambako wanapata matofaa haya madogo baada ya waridi kuisha, na hayo matofaa madogo, na ni kitu cha bei ghali mno, kama yale malkia wa Sheba aliyomletea Sulemani, manukato, nardo, na kadhalika, nao walitengeneza manukato haya kutokana nayo.

¹⁰¹ Nao wakajistarehesha kwa...Walikuwa, miguu ilioshwa, uvundo ulikuwa umewatoka, jua hilo kali, lililosababisha malengelenge usoni mwao, ndipo wakaburudika. Halafu jambo lingine, hatua ya kwanza, hatua ya pili, sasa hatua ya tatu. Sasa, ningeweza kuhubiri juu ya hilo kwa muda kidogo, bali sina wakati, jinsi ambavyo huko ni kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

¹⁰² Ndipo, walipoingia, walikutana na wageni... wakakutana...wakalakiwa na mwe—mwe—mwenyeji. Halafu

kitu kama hiki (Simama, Ndugu Demos.), baada ya, mnaona, kutawadhwa, kupakwa manukato, ali-. . . hakuona aibu kwa sababu ya ule uvundo. Alikuwa amevaa viatu laini vya kutembea juu ya hayo mazulia makubwa ya Kiajemi. Alikuwa amepakwa mafuta, alikuwa na harufu nzuri mwilini, sio ule uvundo wa wanyama, bali alitiwa manukato. Ndipo wakanyosheana mikono *hivi* (Njoo papa hapa, Ndugu Demos.), Nimekuwa huko Mashariki, sasa, chukua mkono *huu* namna *hii*, ndipo wangekuja *huku* pamoja. Ndipo wakapigapigana wenyewe kwa wenyewe kikofi cha upendo wakati mwenyeji alipokutana na mgeni, basi huko kuliitwa kukaribisha. Mnaona, alikuwa ametawadhwa, akatiwa manukato, kisha akakaribishwa kwa busu. Walibusiana shingoni, akakaribishwa kwa busu, basi alikuwa ndugu kamili.

¹⁰³ Hivyo ndivyo ilivyo Kanisani tunapooshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo, tukatiwa manukato na Yungiyungi la Bondeni, na kubusiwa na Baba, ndipo sisi ni wageni waliokaribishwa. Loo, kuna mengi sana ya kusemwa hapo, lakini ili nisiwaweke muda mrefu sana, sitaki kuwachosha.

¹⁰⁴ Lakini wakati, kisha akabusiwa, akakaribishwa, ye—yeye yuko nyumbani, haikumbidi kuhofia chochote. Angeweza kwenda kwenye friji achukue sambusa kubwa, na kuvua viatu vyake, alale kitandani, chochote alichotaka kufanya, alikuwa nyumbani.

¹⁰⁵ Na wakati Mungu anapotukaribisha kwa busu katika Ufalme Wake, tuko Nyumbani, ni sawa, yote yamekwisha basi, tumeoshwa kwa maandalizi aliyotuandalia: Damu Yake, Harufu nzuri ya kепendeza, tumetiwa manukato kwa utakaso unaoondoa uvundo wa ulimwengu (Haleluya! Kwa namna fulani ninajisikia kubarikiwa sasa hivi.), kuondoa uvundo wa ulimwengu, ama tamaa za ulimwengu.

¹⁰⁶ Mnaona, kama ulimwengu ungali ndani yetu basi kuna kasoro fulani. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho halisi wa Kipentekoste, si ajabu kuna kasoro, huyo mgeni hajaingia vizuri kabisa. Mnaona, Yesu alifundisha hilo wakati mmoja kuhusu hayo majoho, Naye akasema, “Mtu huyu alionekana huko hajafanyiwa maandalizi, ndipo akafungwa na kutupwa katika giza la nje.” Mengi sana yangeweza kusemwa juu yake.

¹⁰⁷ Lakini hivyo ndivyo walivyofanya. Basi walikuwa nyumbani, walijisikia kama walikuwa ndugu. Huwezi kujisikia kama wewe ni ndugu wakati ungali unautamani ulimwengu. Huwezi kujihusisha hapa nje katika mambo ya ulimwengu ya kudanganya, kusema uongo, kuiba, ninyi wanawake mnaokata nywele zenu na kuvaa kaptura na kila kitu, halafu mngali mnajisikia nyumbani wakati Neno la Mungu linapohubiriwa. Mnadhaniwa kuwa Pentekoste, mnadhaniwa kuwa mumejazwa na Roho Mtakatifu.

108 Mtu fulani alinishambulia si muda mrefu uliopita, kasema, “Kwa nini usiachane na hao watu?” Kasema, “Watu wanafikiri wewe ni nabii.”

Nikasema, “Mimi si nabii.”

109 Kasema, “Vema, wanafikiri ndivyo ulivyo. Kwa nini usiwafundishe hao watu, hao Wapentekoste, jinsi ya kupokea mambo haya, jinsi ya kupata baraka kuu za kiroho na kuingia Uweponi mwa Mungu na kuona maono pia, kama ungeachana nao.”

Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?”

110 Wanawezaje kukubali mambo ya kiroho wakati hata hawata-...hawana adabu ya kutosha kujisafisha? Sio kuwaumiza, bali kuwa mwaminifu kwenu. Mambo yasiyo ya heshima ambayo Biblia inasema hampaswi kuyafanya, hata hivyo tunajihusisha nayo. Hakika. Unaona, huwezi kukaribishwa, la, bwana. Uko nje ya mahali pako kwa Neno, na Yeye ni Neno. Sasa, hayo yanatosha, tutalipata hilo wakati mwingine. Lakini, angalieni, tunapoendelea.

111 Unasema, “Una shida gani?” Vema, ninyi wanaume mtakaowaacha wafanye hivyo, hilo linaonyesha mmeumbwa kwa kitu gani. Baadhi yenu wanawake, wake za wachungaji, mnafanya hivyo na kuvalia namna hiyo! Ni kitu gani? Mnajaribu...Ati mume wako atakuruhusu ufanye hivyo? Loo, Ndugu! Ni kitu gani? Baadhi ya mitindo hii ya kukata nywele kichwa-maji mliyo nayo, mkijaribu kutenda kama mama taifa wa nchi. Yezebeli alikuwa mama taifa wa nchi, pia! Baadhi ya wachungaji wao wasingewaambia habari zake, bali walikuwa na Eliya kule chini, aliyelitetea vizuri. Huyu alikuwa ndiye mchungaji wake, hakutaka kuamini jambo hilo. Akiongozwa kote...

112 Angalieni, tunaona ya kwamba iliwabidi kuwa tayari na kujiandaa kuingia. Ilitukiaje? Tunamwona sasa, ameketi chumbani, hajatawadhwa, hajapakwa mafuta, hajakaribishwa kwa busu, ameketi katika nyumba ya kadinali. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani: Ilikuwaje kwa huyo mtumishi mtawadha miguu? Alikuwa wapi? Alimkwepaje huyo? Ni fursa ya jinsi gani, naye akaikosa. Loo, ninaamini kama ningalikuwa huko na kujua Yeye alikuwa yuaja, ningekuwa kwenye ngazi ya vipandio mahali fulani, nikimtamazia Yeye kuja. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Heshima ya kuitawadha miguu Yake, ile heshima! Lakini, kwa namna fulani, alimkwepa tu, akamwacha aende.

113 Yule mtu aliyekuwa na mafuta ya kupaka alikuwa wapi? Lakini, kwa namna fulani, Yeye alikuwa pale na alikuwa mchafu. Inaniua kusema hivyo, lakini Yesu akiwa na miguu mchafu. Mnajua Mfaransa anamwita, “Jésus.” Jésus. Jésus

akiwa na miguu michafu, hakuna mtu anamjali, vya kutosha kuiosha miguu Yake.

¹¹⁴ “Hilo linatuhusu nini, Ndugu Branham?” Yeye alikuja wala hakuchelewa, Yeye daima huja kwenye wakati unaofaa, kamwe hachelewi. Tunaombea uamsho, Naye anakuja, mtu fulani anaanza kumsifu Bwana, ama kulia, anafukuzwa kanisani. Mnaona? Hakaribishwi kamwe. Jésus akiwa na miguu michafu.

¹¹⁵ Loo, kwa nini akachafuka? Alichafuka akija kwa kuwa alialikwa kuja. Na siku hizi amealikwa pia, anapokuja anaitwa mtakatifu anayejibingirisha, jina fulani la kikashfa. Kwa nini akachukua kitu kama hicho? Kwa sababu tulimwalika aje, naye Mungu akashuka katika umbo la mwili wa mwanadamu. Aliishi hapa duniani. Alifanyika hivyo ili kwamba . . .

¹¹⁶ Tulimwalika Mungu aje, na halafu anapokuja, hawamtaki. Hawakumtaka. Mara nyingi hatumtaki, inaingilia utaratibu wetu wa kimadhehebu, inaingilia hadhi ya kijamii tuliyo nayo na makanisa mengine. Mungu na aturehemu maskini sisi Mafarisayo, wenye mashaka.

¹¹⁷ Tunachohitaji ni nguvu za Roho Mtakatifu kurudi kwenye majengo, na kurudi ndani ya watu, wapate kuwa na nguvu za Kipentekoste za mtindo wa kale zilizolisafisha kanisa kuanzia bawabu hadi mchungaji. Hiyo ni kweli. Amina. Hilo ndilo tunalohitaji. Lakini tunaziombea, na zinapokuja, “Loo, la! Hilo linaingilia hadhi yangu ya kijamii.” Mnaona? Loo, hakika, linapunguza heshima kidogo. Kama hutalifanya tu *hivi-na-hivi*, watu hawatakuja. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu.” Angalieni tena, “Wote alionipa Baba watakuja.” Dumisha kitu hicho kikiwa safi.

¹¹⁸ Kamwe hatuwezi kujilinganisha na ulimwengu, tunafanya makosa kwa kujaribu kutenda kama ulimwengu. Kamwe hatuwezi kujilinganisha nao, wala hatuna shughuli yoyote huko nje kwenye maeneo yao. Waleteni huku kwenye maeneo yetu, kwani tuna kitu Fulani wasicho nacho. Tukianza kutenda kama wao, basi wanajua tu—tuna—tunasema jambo fulani ambalo hatuna. Acha—acheni ulimwengu uje kwetu, sio sisi kuufuata ulimwengu. Acheni uli- . . .

¹¹⁹ Mnajua, Hollywood hung’aa, bali Injili humeka. Kuna tofauti kubwa sana kati ya kuang’aa na kumeka. Kumeka, sio kung’aa kwa sura ya nje, kumeka kwa ndani kwa Roho Mtakatifu, kwa utamu, upole, unyenyekevu, subira, na upendo. Meka, using’ae. Kung’aa ni kuufuata ulimwengu.

¹²⁰ Kanisa liko zaidi sana kama lilivyokuwa katika siku za Esta. Esta hakuchukua manukato ya hao wanawake, alijipamba kwa mavazi ya kujisetiri, Mtu aliyefichwa wa moyoni, ndipo mfalme akasema, “Mvikeni taji kichwani *mwake*.” Esta alikuwa mfano wa Kanisa siku hizi, wale walio tayari kujitokeza na kujipamba kwa utamu wa Roho Mtakatifu, si kutia manukato

na mapambo ya ulimwengu, kujaribu kujilinganisha nao, bali yule Mtu aliyefichwa wa moyoni, huyo Ndiye.

¹²¹ Angalieni, tunamwona Jésus ameketi huko nje na miguu michafu, kamwe isingonekana. Aliingiaje? Alikosaje...? Yule mtumishi mtawadha miguu alimkosaje? Hao wengine walimkosaje? Sijui. Lakini Yeye alikuwa ameketi pale na miguu michafu, hakuna mtu aliyekuwa akifanya lolote kulihusu. Loo, Farisayo, yeye na huyo mwingine, askofu, na askofu mkuu, na kadinali, na hao wengine wote walikuwa kule wakigonganisha hizo bilauri, na kunywa di—divai nzuri, na—na kuzungumza juu ya mambo ya...ya Israeli, bali walikosa kumwona Mungu wa Israeli.

¹²² Hiyo ni leo hii, tunataka jengo lililo kubwa kuliko yote mjini ama...na watu wote wanapenda kumiminika kwenye jengo kubwa kuliko yote yaliyoko mjini, hawa wote wakubwa, waliovalia nadhifu zaidi, na hawa wengine wote, na maskini mtu mdogo akihubiri Injili huko chini pembeni mwa barabara, ama huko nje mahali fulani kichocho, katika kanisa dogo, nawe hutaki kushirikiana naye. Kuna shida gani? Kuna kasoro. Unaenda kule ambako watu wengine wanatenda *hivi* na kuvaa vizuri zaidi. Ni vibaya sana linaingia katika milki zetu. Kweli.

¹²³ Tunachohitaji ni kujinyenyekeza. Tunachohitaji ni ubatizo wa Roho Mtakatifu tena, pamoja na upendo na nguvu za Mungu kuuondoa ulimwengu huu ndani yetu, kuturudisha kwenye kujipamba tena kwa Neno, tumeosha kwa maji ya Neno. Tumrudie Kristo, badala ya kujifananisha na ulimwengu, kujaribu kutenda kama mama taifa na—na mambo haya mengine yote, baadhi ya maaskofu, na kadhalika, hilo halijalishi, unataka kuwa kama Yesu, Jésus.

¹²⁴ Sasa, wazia jambo hilo, kila mtu akisimama kuzunguka ua baada ya karamu kuanza, harufu nzuri ya mwana-kondoo na—na ninii, kila kitu. Hakukuwako na mtu mtaani, kila mtu alikuwa amesimama, akiangalia ndani, vinywa vyao vikijaa mate, wakiwa na uchu wa kupata kipande cha huyo mwana-kondoo. Wasingeweza kuingia, la, walikuwa maskini, takataka, nje. Na hapa kulikuwako na Mtu humo ndani aliyevalia na kufanana na hao walio nje, kuna kasoro mahali fulani. Ameketi pale, hamna hata adabu tu ya kuitawadha miguu Yake, wala—wala kumkaribisha kwa busu, kaachwa tu aketi pale, hakuna anayemkaribia. Wanafunzi Wake wasingeweza kuja, hawakualikwa. Lakini Huyu hapa, ameketi hapa, akiangalia pande zote.

¹²⁵ Sasa, sikilizeni, huko chini kabisa mtaani, kuelekea sehemu ya chini kabisa ya mji, huko chini kwenye mtaa wa makahaba, tunaingia kulia, tunapanda kwenye kichocho, kuna maskini vipandio kuukuu vinavyotoa mlio vinavyoshukia upande wa nyuma, na unapovipanda, vinatoa mlio mwembamba na kutoa

mlio mwembamba, tunafungua mlango, nasi tunaona mle ndani maskini mwanamke mmoja. Loo, siamini alimaanisha kuwa mbaya, labda alikuwa na mzazi mzuri, naye akachukua tu njia mbaya, ama labda alikuwa msichana mzuri, Yuda fulani mwenye nywele laini za mawimbi akaharibu sifa za maskini msichana huyo.

¹²⁶ Sikuzote ninawakemea wanawake, naenda kuwatetea kwa muda kidogo. Kunao wasichana wengi wazuri waliopotea kwa sababu ya maskini Yuda fulani aliyejitia marashi, akikimbia huku nywele zake zimechanwa chini, na kukipanua kinywa chake mbele, akiendelea na maskini kitu fulani cha, moja ya mitambo hii ya Ricky ama Elvis huku nje mtaani, kutembea na msichana mdogo sababu anafikiri yeye ni mzuri, anampa sigara, anampeleka kwenye dansi.

¹²⁷ Nimekutana na maelfu yao, maskini maisha yao yameharibiwa na kuangamizwa. Sio kosa lao sikuzote. Kamwe usidanganywe na mvulana kama huyo, Dada, achana naye, hana faida endapo hajajazwa na Roho Mtakatifu.

¹²⁸ Nitasema jambo fulani, silikusudii kwa mzaha, maana hapa si mahali pa mizaha, lakini jambo fulani tu lililotukia kanisani mwangu; hapa ni mahali pa Injili. Tulikuwa na msichana mmoja kanisani mwetu hapa wakati fulani uliopita, msichana mdogo mzuri, mrembo, muda si muda mwajua, akakata nywele zake. Hiyo ni kinyume na kanuni. Naam, bwana. Anapofanya hivyo, Biblia inasema yeye ni mwanamke asiye na heshima, achana naye. Biblia ilisema mwanamke, kukata nywele zake ni aibu. Sasa, hilo ni Neno. Mungu anajua hiyo ni kweli.

¹²⁹ Na kama Roho Mtakatifu yuko ndani yako wala hatashirikiana na Hilo, huyo ni Roho Mtakatifu wa aina gani? Roho Mtakatifu, Mwenyewe, ndani yako, anakufanya uishi kile ulicho. Kama Roho Mtakatifu hakubaliani na Neno, nawe unamwita Roho Mtakatifu, basi si Roho Mtakatifu wa Mungu, una namna fulani ya roho.

¹³⁰ Siku hizi tuna kila namna ya roho. Watu wanasema, “Funga macho yako, fungua kinywa chako, pokea kitu fulani.” Kweli unapokea, lakini angalia kile ulichopata baada ya kukipokea. Kamwe usifanye hivyo, wewe mjie Mungu kwa busara, kwa akili zote, ukilishikilia Neno. Mpate Roho wa Mungu, atakufanya utembe sawasawa na Mungu, hakika.

¹³¹ Maskini msichana huyu, alianza kuzurura na maskini Elvis. Baada ya kitambo kidogo nilimwuliza, nikasema, “Martha, ni—ni kitu gani kinachokufanya ufanye hivyo? Unaona nini katika jamaa huyo? Anavuta sigara, nilimwona amesimama moja kwa moja kwenye uwanja wa kanisa akivuta sigara.”

¹³² “Loo,” anasema, “Ndugu Branham,” kasema, “unajua,” kasema, “ana nywele nzuri, za mawimbi,” kisha kasema,

“ananukia tu vizuri sana.” Sasa, kama hilo si jambo la kumchagua mpenzi wa kiume!

¹³³ Nikasema, “Lakini hajaokoka.” Nikasema, “Afadhali niende na mvulana ambaye alinuka kama boma la mifugo, na alikuwa na miguu kama behewa, na awe na Roho Mtakatifu.” Naam, ningefanya hivyo, kuliko moja ya maskini mambo hayo. Hatimaye aliishia kwenye njia mbaya, kama labda maskini msichana huyu alivyofanya. Mvulana fulani alimwongoza vibaya, ndipo akaanza. Na kama tayari umeanza, Dada, kuna matumaini kama tu utakutana na Mtu huyu ninayenena habari zake. Labda hakuwa amepata hiyo nafasi.

¹³⁴ Kwa hiyo anaanza kuteremka mtaani kwa majukumu yake ya kawaida. Wala haoni mtu yeyote. Kwani kila mtu yuko wapi? Kisha anapitia kona nyingine na kona nyingine. Kila mtu yuko wapi? Hakuna mtu leo. Baada ya kitambo kidogo, *nusa*, ananusa harufu hiyo, maskini tumbo tupu linaanza kuona njaa. Anasogea mbele miongoni mwa umati, anapanda karibu na mlango wa Farisayo, naye anamwona askofu, na makadinali, na hao wote mle ndani, wakigongeshana bilauri. Naye anajisukumiza uani, nao watu wanaanza, wanamwondokea, baadhi yao ni wabaya kuliko alivyo yeye. Hiyo ni kweli.

¹³⁵ Wa mtindo wao wenyewe, hawatambui ya kwamba kila mwanamke aliyeenda kombo alikuwa na sababu fulani ya kufanya hivyo, kila mwanamume aliyeenda kombo. Nasi tunafikiri sisi ni wa mtindo wetu wenyewe sana mara nyingi hatutaki kushirikiana na ombaomba mtaani. Hatuna wakati wa kusimama na kuzungumza nao kwa dakika moja. Halafu ati tunajiita Wakristo?

¹³⁶ Naam, alijisukumiza mpaka uani, naye alikuwa akiangalia huku na huko, *akinusa*, alikuwa na njaa. Naye akaangalia, naye alikuwa akiangalia, *hapa* pembeni alisimama yule Farisayo, angeweza kusikia ile “Ho-ho-ho-ho” kubwa mno, huko pembeni, akaangalia huku naye huyu *hapa* akigonganisha bilauri zenye divai ile nzuri, ya kupendeza, na mwana-kondoo akichomwa, na chakula cha jioni kikiwa karibu kuandaliwa.

¹³⁷ Na—na huku akiangalia pande zote namna hiyo, ndipo baada ya kitambo kidogo macho yake yakamwona Mtu fulani (Loo, sote na tuishike picha hiyo sasa.), ameketi pale pembeni, hawamjali, naye hapana shaka alionekana Naye. Hakuna mtu anayeweza kumtazama Yeye machoni anayeweza kuhisi vile vile tena. Alimwona, naye akawaza, “Ni nani Yule? Kuna kitu tofauti kumhusu.” Na kipo. Kamwe hapajakuwapo na mtu kama Yeye, kamwe hakuwezi kuwa na mtu kama Yeye. Alikuwa tofauti na wengine. Naye huyo hapo ameketi, akaangalia chini, nao watu walikuwa, walimwondokea. Nao... Aliona miguu Yake ilikuwa haijatawadhwaa, uso Wake ulikuwa ungali umekauka na unafukuta.

138 Laiti tungaliweza tu kuona jambo hilo leo, nanyi mnajua ninalozungumzia, kumwona Yeye ameketi katika aibu, kama watu Wake wafanyavyo siku hizi kwa walimwengu, hawataki kabisa kujihusisha nao. Wao ni sawa na... Unasema, "Pentekoste," ndugu, wamekwisha. Unasema, "Roho Mtakatifu," loo, jamani, wako mbali Naye.

139 Tunachohitaji sisi watu kufanya ni kumwosha miguu, kumpaka mafuta, tupate kuinuka katika nguvu za kufufuka Kwake, kumwondolea aibu hiyo. Amina. Kuwafanya walimwengu kujionea aibu, tukiwa na nguvu za Uhai Wake ndani yetu, kama viumbe tofauti, si kama wao huko nje, hao ni chakula cha mizinga, hao si kitu ila majivu ya atomiki, Kanisa ni Kiumbe kilichozaliwa mara ya pili.

140 Huyu hapa ameketi. Katika umati wa aina hiyo hivyo ndivyo anavyoonekana. Na hivyo ndivyo mwanamume ama mwanamke aliyejazwa na Roho halisi anavyoonekana mbele ya umati kama huo. Angalia, alimwangalia, akawaza, "Unajua yule ni Nani?" "Mtu fulani hapa... Je, Yule ni Nabii yule wa Galilaya?"

"Loo, huyo ni Yeye."

141 Loo, moyo wake ukaanza kudundadunda. Jambo fulani, unapompata Yesu, moyo wako unaanza kutenda mambo ya kipekee, huo utampata Bwana mpya mara moja. Moyo ukaanza kudundadunda, "Loo, huyo—huyo Ndiye aliyekuwa kule chini kisimani alikokuwa yule mwanamke wa Sikari. Huyo Ndiye aliyekutana na huyo mwanamke mtovu wa uadilifu kama mimi, na kumwambia ya kwamba alikuwa na waume wengi kupita kiasi, na kumsamehe, dhambi zake. Loo, Yeye kamwe asingenisamehe, mimi ni mbaya sana. Lakini si vizuri Yeye kuketi pale namna hiyo, Yeye ni Mungu wa Umilele, Yeye ndiye Mwokozi pekee, si halali atendewe hivyo." Ndipo akapata wazo. Natumaini utapata moja.

142 Huyu akashuka mtaani, haraka tu kadiri awezavyo, akashuka kwenye hicho kichocho kidogo, akapanda kichocho akavifikia maskini vile vipandio vinavyolia. *Kung-kung, kung-kung*, huyo anapanda, anaufungua ule mlango mdogo unaopiga kelele nyembamba, baada ya kuondoa kufuli, anaingia, anaanguka sakafuni, anawazia, "Nimepiga magoti." Ananyosha mkono wake chini ya kitanda, anachomoa kijisanduku kidogo, kisha anakifungua, na maskini soksi yake ndefu, labda, anaitoa, anaitikisa, hiyo hapo riziki yake yote. Hizo tu ndizo alizo nazo, bali yuko tayari kuzitoa.

143 Sijui kama sisi ni waaminifu hivyo. Usimnyoshee kidole kama sivyo ulivyo. Zote alizokuwa nazo, alikuwa tayari kuzitoa. Naye anaziweka kifuraha mwake, huku yeye, moyo wake umejaa furaha. Mara, kitu fulani kinawasilishwa kwake: "Unajua, Yeye ni Nabii, ninaamini Yeye ni Nabii. Sijali yale rabi asemayo, yale kadinali, ama askofu asemayo, ninaamini ya kwamba Yeye

Ndiye ambaye Musa alinena habari zake. Ninaamini ya kwamba Yeye ndiye yule Nabii aliyekuwa atuzuru katika siku hizi. Naye akiwa Ndiye, atajua mahali nilipopata pesa hizi, Yeye atajua mbi—mbinu nilizotumia kupata pesa hizi, bali ndizo zote nilizo nazo.”

¹⁴⁴ Hakika Yeye anakujua. Anaweza kukwambia moja kwa moja kwenye mimbara hii sasa hivi yote kukuhusu wewe. Naam, bwana. Mnaamini hilo? Ninaweza kuwathibitishia. Amina. (Samahani.) Anajua umeumbwa kwa kitu gani. Anajua maneno haya wakati mwingine hukuchoma. Anajua yote kukuhusu.

¹⁴⁵ Lakini ni yote aliyokuwa nayo. Hayo ndiyo yote anayotarajia kutoka kwako, mtolee tu yote uliyo nayo, moyo wako wote, mapenzi, na umaarufu, hadhi ya kijamii, mtupie tu yote, haidhuru umefanya nini. Lakini akasema, “Hii ndiyo nafasi yangu ya pekee, nami nitaichukua.” Labda huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho, afadhali uichukue wakati ukiwa katika mkutano huu, usiende nyumbani bila hiyo, kwa kuwa ninaamini utamwona akitenda kazi vivyo hivyo, tayari anatenda, utamwona Yeye akiwa mkuu kuliko hivi, utaona Neno Lake likidhihirishwa.

¹⁴⁶ Angalieni, naye anasema, “Ndiyo yote niliyo nayo, kwa hiyo ndiyo yote ninayoweza kutoa.” Hayo tu ndiyo anayotarajia. “Ndugu Branham, mimi ni—mimi ni. . .” Sijali wewe ni nini, umekuwa mnafiki kiasi gani, jinsi umekuwa mfuasi mzuri wa kanisa, jinsi unavyoweza kusimama ukijidai mwenye haki asubuhi ya leo mbele za watu, toa tu kile ulicho nacho, hicho tu ndicho anachotarajia, atachukua hicho.

¹⁴⁷ Anashuka mtaani, akasema, “Vema, rahisi, nitaenda kwa sababu kuna Kitu fulani ndani yangu kinachoniambia nifanye hivyo.” Huo ndio wakati ambapo ni halisi, si wakati unapojifanya, bali kitu halisi. Huyu hapa anashuka mtaani, naye anaangalia pande zote, naye akakumbuka Lavinsky ana duka bora zaidi la manukato mjini.

¹⁴⁸ Kwa hiyo anaingia mlangoni, hiyo kengele ndogo inalia na mtu mmoja akasimama, akaangalia aone ilikuwa ni nani, “Vema, unataka nini?” Kama vile baadhi ya watu hawa kabla hawajawa wafanyabiashara Wakristo, hiyo ni biashara duni.

“Unataka nini? *Sipendi mtu kama huyo kuwa kwenye duka langu.*”

“Nataka yaliyo bora sana uliyo nayo.” Loo, jamani!

“Ati bora sana niliyo nayo?”

“Naam. Ni kwa ajili ya—ni kwa ajili ya Mtu fulani halisi. Ni kwa ajili ya hafla maalum.”

¹⁴⁹ Hivyo ndivyo tunavyotaka, yaliyo bora zaidi yanayoweza kupatikana, yaliyo bora zaidi tunayoweza kutoa, si dakika tatu tu kwa siku katika maombi, bali bora sana uwezayo kutoa. “Loo,

nataka yaliyo bora sana uliyo nayo!” Vema, alijua mwanamke kama huyo kweli hakuwa na pesa za kutosha kununua hayo. Kwa hiyo anafungua kifuniko cha maskini stokingi yake na kusema, “Yaliyo bora sana ni pesa ngapi?”

“Vipande ishirini, hayo ndiyo bora sana niliyo nayo.”

¹⁵⁰ Anamiminia maskini soksi yake hapo juu, nazo hizo pesa zinachacharika. Loo, bila shaka, hiyo ni tofauti. Yeye aliyesema hakuna faida katika kumweka Yusufu nchini, yeye yuko tayari kufaulu mwajua. Kwa hiyo anapanda pale na kuzihesabu, “Loo, naam, vipande ishirini hasa vya dinari za Kirumi, hiyo ndiyo bei yake. Unaenda kufanya nini na haya?”

“Loo, haya ni kwa ajili ya Mtu maalum.”

¹⁵¹ Kwa hiyo akanyosha mkono kwenye rafu na kumpa kile kibweta cha marhamu. Akakiweka kifuani mwake. Anarudi tena haraka, anaangalia mle ndani, anamwona Farisayo na hao wote wamesimama pande zote katika mkusanyiko mkubwa sana wa—wa fahari. Kisha anamwona Jésus angali ameketi pale na miguu michafu, hakuna aliyekuwa amemjali. “Nitaingiaje? Watanitupa nje nitakapoelekea langoni.” Lakini mnajua, kuna kitu Fulani ndani yake, kinachomwambia aingie, alitaka kumtumikia Yesu.

¹⁵² Na kama unataka kumtumikia Yesu, hakuna maaskofu na makadinali wa kutosha duniani kukuzuia kwenda Mbele Zake. Hiyo ni kweli. Hakuna madhehebu ya kutosha na wanafiki nchini wa kufanya hivyo, ama pepo wa kutosha kuzimuni kukuzuia, kama unataka kumtumikia Jésus.

¹⁵³ Huyu hapa anakuja, ananyemelea, anamwona mlinzi langoni amempa kisogo, anaingia kisiri chini ya lango, hapa anapita upesi sana. Hiyo ni kweli. Unapoingia kwa mara ya kwanza, mwendee moja kwa moja, usifanye fujo. Usiende ukizungumza, kuangalia yale *huyu* asemayo, na yale dhehebu *hili* lisemayo, na *lile* linasemayo, nenda moja kwa moja kwa Yesu. Nenda kwa Jésus! Usijali yale hawa wengine wasemayo, mwendee upesi.

¹⁵⁴ Kwa hiyo anaingia kisiri upesi sana, anasimama, Biblia ilisema, nyuma Yake, akaanza kuwazia, “Loo, loo, niko Mbele za Mungu!” Hisia ya ajabu sikuzote huja juu yako unapokuja katika mtazamo huo. Lakini kama ukija katika mtazamo aliokuwa nao Farisayo huyo, utakuwa na hisia ile ile aliyokuwa nayo: haina faida. Lakini njoo tu katika msimamo huo kwamba unataka kumwona Jésus, uone ni hisia ya aina gani inayokuja juu yako. Hebu maskini moyo huo uyeyuke ndani yako asubuhi ya leo kumwelekea Yeye. Sikiliza Sauti Yake ndogo tulivu, kutakuwa na mtazamo tofauti.

¹⁵⁵ Anaingia kisiri, Yeye alikuwa ameketi pale, akawaza, “Loo, loo, nina wasiwasi sana, sijui la kufanya. Kama nikikaribia hapa, huenda Yeye labda akanifukuza hapa. Loo, nini...? Vema, mimi si ki-. . . mimi si kitu hata hivyo.” Sasa, unapoanza

kuwazia hilo, wewe si kitu kwa vyovyote vile! Kama unahofu utaharibu heshima yako, basi kwanza kabisa afadhali ukae mbali. “Kwanza kabisa mimi si kitu.”

¹⁵⁶ Kwa hiyo akakimbia mbele Zake na kuangalia, ndipo akawa karibu. Hapo ndipo unapotaka kufikia, kukaribia tu kidogo upate kumtazama Yeye. Labda unamwangelilia kwa mbali mno, unamwangelia Yeye huko nyuma kabisa, miaka elfu mbili iliyopita, vipi kuhusu Yeye asubuhi ya leo? Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele; nguvu zile zile, ishara zile zile, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

¹⁵⁷ Ndugu Demos muda mfupi uliopita alilinkuu katika King James, “Kubwa kuliko hizi mtafanya,” lakini tafsiri sahihi, na mtu yeyote anajua, ni “*Nyingi* kuliko hizi mtafanya.” Si *kubwa zaidi*, hakuna mtu angaliweza kufanya kubwa zaidi, bali nyingi zaidi ya kazi zile zile kuu. Aliwafufua wafu na kuyakomesha maumbile, hakuna kitu kingine kikubwa zaidi kingaliweza kufanywa, ila nyingi zaidi. Kwa nini? Yeye yuko katika Kanisa Lake la ulimwenguni kote, lile Kanisa kuu la katoliki takatifu, la kimitume, la Kipentekoste, kote ulimwenguni, Jésus ndani ya kila mshiriki.

¹⁵⁸ Yeye alikuwa ndani ya Mtu mmoja tu, Mungu alikuwa wakati huo, sasa Mungu yuko ndani ya Kanisa Lake lote. Saa ii hii watu wanaponywa, dakika ii hii watu wanampokea Roho Mtakatifu. Kama alikuwa tu amesimama hapa peke yake katika umbo la mwanadamu kama alivyokuwa wakati huo, angalikuwa tu akizungumza na kusanyiko hili, lakini sasa Yeye anazungumza ulimwenguni kote katika Roho Mtakatifu.

¹⁵⁹ Kwa hiyo huyo hapo katika Uwepo Wake, akatembea kote. Ninaweza kuona hayo macho madogo yakimwangelia, na moyo wake karibu uzimie, “Huyo hapo yule Mtu aliyemsamehe mwanamke huyo na kuujua moyo wake. Alimjua mwanamke yule wa Samaria, Sikari. Yeye—Yeye alijua mwanamke huyo alikuwa na waume watano, Naye anajua jinsi nilivyo na hatia.” Yeye anajua, anajua jinsi ulivyo na hatia. Yeye anajua jinsi kila mmoja wetu alivyo duni, Yeye anatumia.

¹⁶⁰ Naye mwanamke akamtazama usoni, ndipo akatambua jambo hilo. Sasa, kamwe hakumwangelia yule Farisayo, wala kuangalia ile chati, na kuona hilo kanisa lilikuwa na wafuasi wangapi, kama angejiunga nalo au la, alimtazama Jésus. Akajisikia mwenye hatia, wala asingeweza kuyazuia machozi yake tena, kisha akaangalia chini miguuni Mwake, nayo machozi yakaanza kutiririka juu ya miguu Yake. Aliona aibu sana, akaanguka magotini mwake, yeye. . . Yeye akamwona, wala asingeweza kuzuia machozi yake tena.

¹⁶¹ Kuna jambo *moja ama lingine* kuhusu wakati unapomkaribia Yesu, unaanza kulia, si kwa ninii bari- . . . Sina haja na maungamo haya baridi, magumu, na kuandika jina

lako kwenye kitabu na k'jiunga na kanisa, huna budi kufa kwa nafsi yako, kuzaliwa upya.

¹⁶² Ndipo machozi yakaanza kutiririkia miguuni mwa Yesu, naye hakuwa na kitu cha kuyapangusia, kwa hiyo huku akiinamisha kichwa chake chini, akilia, nywele za—za—zake nzuri zilizopindana alizokuwa amezitengeneza juu ya kichwa chake, mwajua, namna *hii*, zikaanguka chini, akaanza kuitawadha miguu Yake kwa mikono yake na—na kuipangusa kwa nywele za—zake. Baadhi ya dada zetu wa Kipentekoste, huku wakikata nywele zao zote nzuri, inawabidi kusimama kwa kichwa chao kupata nywele za kutosha kuitawadha miguu Yake. . . kuipangusa. Kweli.

¹⁶³ Lakini Yeye . . . yeye, hata katika hali yake . . . Usimhukumu! Alishika nywele zake, akaanza kuipangusa miguu Yake, naye angeangalia juu. Loo, kama angaliusogeza mguu, kama yeye . . . kama Yeye angalipepesa jicho, *angefyuu* aondoke hapo. Lakini Jésus, unapojaribu kumfanyia jambo fulani, Yeye anakuacha tu ulifanye; ninapenda hilo. Aliketi tu kimya na kumwangalia.

¹⁶⁴ Naye, alijaribu kusema, “Mi—mi—mimi . . .” huku anaipangusa miguu Yake, “Mimi . . .” Ni maji mazuri jinsi gani ya kuitawadha miguu Yake! Machozi ya toba, yaliyo bora kuliko angaliweza kupata kutoka kwa maskini Farisayo, maskini maji ya kimadhehebu ya kujitengeneza, alikuwa na maji ya toba, machozi yake makubwa mno yenye chumvi yakiipiga miguu Yake. Yeye, huku akiosha tu na kuipangusa miguu yake kwa nywele zake nzuri, akisema, “Mimi—mimi . . . Loo, siwezi kulisema.” Alikuwa, “Mimi—mimi . . .” huku akiipangusa miguu Yake. Ndipo i—i—ikawa halisi sana, akafanya, “*busu, busu*, Loo, siwezi kulisema.”

¹⁶⁵ Jamani! Jésus alimtizama tu. Baada ya kitambo kidogo akatoa kile kibweta cha marhamu. Aliona aibu kusimama apate kumpaka kichwani Mwake, a—akawazia, “Kama ninaweza tu kuketi miguuni Pake, hilo litakuwa zuri vya kutosha.”

¹⁶⁶ Baadhi yenu mnataka kuwa watu mashuhuri, miguuni Pake ni pazuri vya kutosha kwangu. Neno Lake latosha. Mradi tu ninajua ya kwamba niko ndani Yake, na Neno Lake ndani yangu, hilo linatosha. Nitakapofika Kule, kama ninaweza tu kuweka mikono yangu juu ya miguu Yake, hilo—hilo latosha, hilo litakuwa sawa, hilo tu ndilo ninaloomba; nafikiri hivyo ndivyo sote tunavyojisikia. Kuosha miguu Yake, machozi ya maji ya toba, hayo ndiyo anayotaka uchafu Wa—Wake uoshwe kwayo, kitubio, si kitubio, toba.

¹⁶⁷ Akiiosha miguu Yake, akiipangusa kwa nywele zake, moja kwa moja akanyosha mkono wake kwa wasiwasi, kisha akakitoa kile kibweta cha marhamu, naye akakigonga, alikuwa na wasiwasi sana, basi akakivunja nchani mwake, akayamwaga yote miguuni Mwake, naye alikuwa na wasiwasi sana, ndi—ndipo

basi akarudi nyuma, na kuanza kuipangusa miguu Yake na, “*busu, busu, busu, busu, busu*, na—na—nataka kuninii . . .” Ndipo akaangalia juu.

168 Aliona macho Yake hayakuwa yakimwangala wakati huo. Ni kitu gani kinachoendelea wakati wote chumbani? Hakuna hatua iliyopigwa. Kuna shida gani? Kila kitu kikasimama. Loo, ninaweza kumwona yule Farisayo mwenye mtindo wa kikwake, laghai katili sana nchini. Loo, yeye ni mwekundu usoni, ameaibika sana, mtu fulani akasema, “Amina.”

169 Mbona, mtu fulani akisema, “Amina,” kanisani mwake, “Ahem!” U—unamsumbua. Nguvu kidogo za Mungu, itokee aseme neno, alikosea mahali fulani, na kusema, “Yesu Kristo alikuja kuwaokoa wenye dhambi.” Ndipo mtu aseme, “Utukufu kwa Mungu!”

“Loo! Ahem! Enyi mabawabu, watoeni nje.” Naam, “Wananisumbua.” Mimi wananisumbua wasipolisema.

170 Kwa hiyo hapo, alidhalilishwa sana, loo, moja kwa moja mpaka, loo, alikuwa tu. . . Loo, rehema, sina budi kumalizia, mnaona. Alidhalilishwa sana. Alikuwa akimwangalia, naye akasema moyoni mwake, akiwaashiria hao makadinali kwa kichwa, “Mnaona? Niliwaambia. Kama mtu huyo alikuwa ni nabii, angejua huyo alikuwa ni mwanamke wa aina gani.” Hakika, Yeye alijua.

171 Alikuwa na hali bora mara milioni moja kuliko yeye, ingawa alikuwa ni mfuasi wa kanisa, yeye alikuwa ni kahaba. Aibu kwenu ninyi washiriki wa kanisa wenye mashaka, wasiomjua Mungu zaidi ya hapo! Akidhalilishwa, kasema, “Niliwaambia, niliwaambia. Mnaona? Kama angekuwa nabii, kama angekuwa nabii, angejua hilo. Yeye si nabii.”

172 Lakini Yesu aliweza kuyatambua mawazo yake, kwa hiyo akajiinua Mwenyewe. Maskini huyo mwanamke akasimama, nywele zake zikining’inia chini, juu ya mabega yake, kufikia karibu kwenye kiuno chake, machozi yanatiririka chini, na—na grisi kinywani mwake mwote kutokana na kuibusu miguu Yake, macho makubwa mno ya kupendeza ya hudhurungi. Sijui atasema nini. Anamwangalia chini.

173 Akasema, “Simoni, nina jambo la kukuzungumzia.” Loo! Maskini mnafiki wa mtindo wa kibinafsi, mwenye mashaka, anayekiri kuwa mtumishi wa Kristo! “Nina jambo la kukwambia. Ulinialika kuja hapa, nami nikaja, nikaacha ratiba Yangu yenye shughuli nyingi.” Yeye hufanya hivyo daima. Hiyo ni kweli. Alikuwa hapa, Yeye yupo hapa sasa, hakika. “Niliacha ratiba Yangu yenye shughuli nyingi kwa sababu ulinialika nje. Ndipo nilipofika mlangoni hukuniosha miguu Yangu, hakunipaka mafuta kichwa Changu, wala hukuniaribisha kwa busu, lakini mwanamke huyu, tangu amekuwa hapa, hajafanya

lingine ila kuiosha miguu Yangu kwa machozi na kuipangusa kwa nywele zake, yeye alinipaka mafuta.”

¹⁷⁴ Sasa, Yeye atafanya nini? Huyo hapo amesimama pale, macho yake makubwa yakimtazama Yeye. Uamuzi ni upi? Ee Mungu, jalia huo uwe uamuzi wangu. Jalia hilo liwe ndilo ninalosikia ninapojaribu kumtumikia, ingawa inanibidi kuwaambia watu wangu mambo ambayo yananikata vipandevipande kwa ndani, lakini sina budi kumtumikia Yeye. Imeandikwa katika Neno, sina budi kuifanya. Hatuna budi kuifanya, ndugu, haidhuru itagharimu nini, hatuna budi kuifanya. Ni huduma ambayo Mungu anahitaji, “Lihubiri Neno.” Kweli.

¹⁷⁵ Mwangalieni, alipigwa na bumbuwazi. “Atafanya nini, kunihukumu?”

¹⁷⁶ Ndipo akaangalia na kusema, “Nami namwambia, dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, amesamehewa zote. Dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, amesamehewa zote.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Huo ndio uamuzi ninaotaka kusikia. Ninataka kujaribu maishani mwangu kufanya kazi ya Mungu, ninyi mnataka kujaribu vivyo hivyo, nao ule uamuzi mwishoni utakuwa ni kitu kile kile, “Dhambi zako, ambazo ni nyingi, umesamehewa zote.”

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

¹⁷⁷ Tumemwalika, Naye amekuja. Kote katika makanisa juma hili pamoja na ndugu zangu, tuliomba, “Yesu, uwe hapa.” Nilisimama juu ya Mlima Kusini hivi majuzi, nikamwambia mke wangu, “Angalia chini kupitia bonde hilo. Ni mara ngapi katika hii saa ya mwisho Jina la Mungu limetajwa bure? Ni mara ngapi uzinzi umefanyawa tangu jana usiku, katika bonde hilo?”

Naye akaniambia, “Billy, ni-. . . ulikuja hapa kwa sababu gani basi?”

¹⁷⁸ Nikasema, “Mpenzi, lakini chini kote kwenye Bonde hilo kubwa la Maricopa, ambamo siku moja hakukuwako na kitu ila mipungate na mijusi, kumekuwa na maombi mengi yaliyoenda juu katika saa ishirini na nne zilizopita, watakatifu halisi wa Mungu waliozaliwa mara ya pili, wanaomba ya kwamba mwenye dhambi atahudhuria mkutano huu.”

¹⁷⁹ Naye amekuja, Yeye yupo hapa, ninajua Yupo. Hebu na tumkaribishe kwa machozi yetu machache kutoka kwenye mioyo yetu baridi na migumu, hebu na tuitawadhe miguu Yake asubuhi ya leo. Hebu tumwambie tunampenda, tutamtumikia tangu sasa na kuendelea, tukasikie uamuzi huo mkuu wa Milele, “Dhambi zako, ambazo ni nyingi, umesamehewa zote.”

¹⁸⁰ Nitawaulizeni swali zito, ninalitaka kutoka moyoni mwenu. Kama kuna wanaume na wanawake hapa, ambao wapo, ambao hawajaiishi sawa na Mungu, nawe ungetaka kusikia ule

uamuzi ambao mwanamke huyo alisikia siku hiyo, “Dhambi zako, ambazo zilikuwa nyingi, umesamehewa zote,” utainua mkono wako? Sasa, mtu yeyote asiangalie, hebu mimi na Bwana tuangalie. Inua mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki, akubariki, akubariki, kote huku.

¹⁸¹ Sasa, enyi washiriki wa kanisa, ninyi hapa mnaojua ya kwamba kamwe hamjawahi kuzaliwa mara ya pili, na hata hivyo Jésus yupo hapa, unajua ungeona aibu kama ingetokea akufanye upaze sauti kumsifu Yeye, ama kujaribu kukwambia umshuhudie mtu fulani, wewe inua mkono wako, useme, “Jésus, samahani, ninataka kuwa Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili tangu leo.” Inua mkono wako. Ubarikiwe, Mungu akubariki.

¹⁸² Sasa, baadhi yenu wanawake wa Kipentekoste wenye nywele fupi, zilizokatwa, aibu kwenu, sasa, mnajua mko makosani. Kama hukujua mpaka sasa, unajua sasa. Unalionea aibu? Kama unaona, inua mkono wako. Mtu awaye yote asiangalie. Mungu akubariki, hilo linahitaji mama halisi kufanya hivyo. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Mungu awabariki. Hiyo ni kweli. Hakika mnaona, hakika mnaona aibu.

¹⁸³ Mnataka kuniambia ya kwamba mmekata nywele wala humjionei aibu? Mkijaribu kuwapendeza wanaume badala ya Mungu? Hivi hamtambui ya kwamba maadamu hamnini. . . ? Kamwe hamtaweza, tangu leo na kuendelea, kwenda mbele zaidi pamoja na Mungu, hiki ndicho kitu kinachowapita, papa hapa.

¹⁸⁴ Ati wasema una Roho Mtakatifu, unacheza katika Roho, kunena kwa lugha? Umetegemea hayo sana, badala ya ile Sauti ndogo tulivu. Unaweza kuwa na mihemuko ya kiakili, lakini maisha yako yanathibitisha kile ulicho. Je, unaweza kupata zabibu kwenye boga? matango kwenye mtikiti maji? Unajua umekosea. Inua mkono wako, uwe *mama* vya kutosha kufanya hivyo. Wengi wenu hamjainua mkono wenu, wengi wenu. . . Mungu awabariki, wako wengi sasa.

¹⁸⁵ Ninyi wanaume mlioruhusu, baadhi yenu wahubiri, aibu kwenu! Ninyi wahubiri wa Full Gospel mnaowaacha wake zenu kufanya jambo kama hilo, aibu kwenu! Mungu airehemu nafsi yako, Ndugu, usiye na adabu ya kutosha kuihubiri Injili. Unamwogopa huyo mwanamke?

¹⁸⁶ Vipi kuhusu baadhi yenu mnaovuta sigara, mngali mnadai kuwa Wapentekoste, mngali mnakunywa kileo pamoja na bosu? Baadhi yenu ninyi wafanyabiashara bado hamjaacha mambo yenu ya ulimwengu, kuninii, mnataka kuninii, hamna budi kunywa kileo kidogo katika Krismasi, aibu kwenu! Aibu kwenu! Kwani hamjui Jésus atawahukumu kwenye siku hiyo? Mnajua mmekosea.

¹⁸⁷ Baadhi yenu hata mmelikwepa Neno katika siku hizi za mwisho. Makanisa yanakuwa ya kawaida, kuna kasoro. Kusanyiko lako halitatetea. . . Ninajua baadhi yenu wahubiri

hamna hatia, mnatoka nje hapa, mnalihubiri Neno kwa bidii mwezavyo, kusanyiko hilo... Lishindilie, Ndugu, Mungu atawawajibisha.

¹⁸⁸ Baadhi yenu hamjampenda Yeye jinsi mnavyopaswa, baadhi yenu ni Wakristo waheshimiwa kweli, wala hamjampenda Yeye jinsi mnavyopaswa kumpenda, nanyi mnajua mna hatia. Hamwombi vya kutosha. Nitainua mkono wangu sasa, siombi vya kutosha, ninajionea aibu, ninayaonea aibu maisha yangu. Nilimwomba aje kwenye mkutano huu, nami ninaninii... ni—ninayaonea aibu maisha yangu mbele Zake. Niko pamoja nanyi, ninayaonea aibu maisha yangu mbele za Jésus.

¹⁸⁹ Namtakia heri, Yeye alikuja kutoka Mbinguni asubuhi ya leo kututembelea, akaja kwetu kuongea nasi, kuzungumza nasi, Yeye anatuzungumzia sasa hivi, ile Sauti ndogo tulivu chini moyoni mwetu. Huenda kusiwe na upepo mkali, unaoenda kasi, tumekuwa na mwingi sana wa huo.

¹⁹⁰ Hebu na tufunike uso wetu asubuhi ya leo kwa aibu. Ninajionea aibu kuwa Mpentekoste kwa maisha ninayoishi, ninaona aibu sina nguvu tena Mbele Zake, ninaona aibu kwamba mimi si mfano wa Mkristo tena mbele za watu wangu. Jésus, unirehemu. Mungu, si kwamba sina kosa, ninahitaji kusahihishwa pia, na Roho Wako Mtakatifu anazungumza nami.

¹⁹¹ Tunataka kuzungumza na Wewe, Bwana, tunataka utusamehe, tunataka kuwa Wapentekoste halisi, Bwana, tunataka kujazwa kabisa na Roho. Hatuyaonei haya machozi, hatukuonei haya kwa njia yoyote, na asubuhi ya leo Wewe umetutembelea, nasi tunataka kutawadha miguu Yako. Tunataka kukupa Wewe maisha yetu, tu—tunataka kuwa Wakristo halisi. Tunataka tunda la Roho maishani mwetu, wapole, wanyenyekevu, tukipendana sisi kwa sisi, tukisameheana. Mungu, kwa ajili ya Kristo, alitusamehe. Tunataka kuwa kama Yeye, Yeye alikuwa Mfano wetu.

¹⁹² Wote walio na shauku hiyo moyoni mwao, kwamba ungetaka tu kuinamisha kichwa chako asubuhi ya leo Mbele Zake, ukijua ya kwamba sisi pia tuna hatia, kwamba ungetaka tu kumtawadha miguu Yake pia, waweza kusimama kimya kwa miguu yako sasa? Mbarikiwe.

¹⁹³ Mke wangu alizoea kuimba wimbo: “Yesu mpendwa, nakupenda, nakupenda Baba. Kama niliwahi kukupenda, Mpendwa Yesu, ni sasa.”

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kila mtu.

¹⁹⁴ Baba yetu wa Mbinguni, [Mwanamke fulani anaanza kulia kwa sauti kuu—Mh.] tu—tumekuwa hatu—hatukujali sana, tumekutendea mabaya, tumeitendea mabaya huduma, tumekuwa wasiojali. Ninamwomba maskini mwanamke huyo sasa hivi, ambaye, ibilisi akijaribu kumwondosha. Mfuatilie, Roho Mtakatifu. Usimwache peke yake, mfuatilie, Yesu. Huyu

ibilisi anayelia, jalia atoke, katika Jina la Bwana Yesu. Jalia maskini nafsi hiyo iliyopotea iokolewe.

¹⁹⁵ Samahani, Bwana. Tenda kazi juu yetu kwa Roho Wako Mtakatifu, tujaze na wema wa Mungu. Mimina baraka Zako, Bwana. Tuna—tunaosha mioyo yetu kwa Maji ya Neno. Ingia maishani mwetu, Bwana, keti mezani petu, keti na ule pamoja nasi leo, Bwana. Tutakuchukua sasa hivi kama Mwokozi wetu, tutakuchukua Wewe kama Kiongozi wetu na Mfalme wetu. Na jalia Roho Mtakatifu azioshe tu nafsi zetu katika Uwepo Wake, akitupa upendo, na rehema, na ufahamu.

¹⁹⁶ Jalia kila mhudumu achukue nafasi mpya. Jalia Wafanyabiashara, naomba madhehebu haya, kila mshiriki wa kanisa, kila mtu humu ndani amhisi Yesu akichukua mahali Pake moyoni mwao sasa hivi. Tujalie, Bwana. Tunakupenda na kukupa maisha yetu, tunakukaribisha mkutanoni. Tutawabatiza watu hapa nje alasiri ya leo, tutafanya miito ya madhabahuni, tutakusifu katika nyimbo, tutakusifu katika Neno, tutakusifu kwa yote tuliyo nayo, kuwafanya watu wajue ya kwamba hatuionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni uweza wa Mungu uletao wokovu.

¹⁹⁷ Tunapaswa kuondoka hapa tukiishi maisha tofauti kwa sababu ya Wewe kututembelea. Hatutajaribu kuwa kama Farisayo, tunajua ya kwamba Wewe ni . . . Mfalme wa manabii, Wewe ni Mungu-Nabii anayenena mioyoni mwetu sasa. Nasi tunaomba ya kwamba utaitambua mioyo yetu, na kutufunulia sababu zetu ambazo zinauzuia ule mwenendo mkuu wa Mungu katika siku hii ya mwisho, ili kwamba kutoka hapa watokee wahudumu waliotiwa mafuta, wanaume na wanawake waliotiwa mafuta sana wakiwa na uvuvio *mkubwa* sana juu yao wa Bwana Yesu mwenye upendo, mpaka kutakuwa na uamsho utakaotokea kote kote katika bara hili. Tujalie, Bwana.

¹⁹⁸ Tunajua Wewe unakuja kwa mwaliko wetu, nasi tutakukaribisha kadiri tujuavyo katika kila moja ya maisha yetu. Tunasimama tukiwa na baraka hii moyoni mwetu, Bwana, tukisema ya kwamba tunakupenda, Bwana Yesu, tunakubariki, Wewe uko juu ya kila—kila shirika, Wewe uko juu ya mambo ya ulimwengu, Wewe uko juu ya mavazi yetu, Wewe uko juu ya vyote vyetu, Wewe ni Mungu, Wewe uko juu ya hisia zetu, Wewe ni Mungu, nasi tunakupenda kwa mioyo yetu yote.

¹⁹⁹ Utupokee, Ee Bwana, tunapokuinulia Wewe mikono yetu kukupa sifa. Yule Mfalme mkuu wa Utukufu ameketi miongoni mwetu asubuhi ya leo. Tunakusifu na kujikabidhi Kwako. Kupitia Jina la Bwana Yesu, tunawabariki watu hawa.

²⁰⁰ Mnapenda? Mnyaweka wakfu tena maisha yenu Kwake, Wanaume kwa Wanawake? Inueni mikono yenu na kusema, “Yesu, niliomba, pia, ya kwamba Wewe ungekuja kwenye mkutano huu, sasa ninajiweka wakfu Kwako, tangu saa


hii na kuendelea jalia niwe Wako kabisa. Jalia kutembea kwangu, kuzungumza, na ushirika wangu uthibitishe ya kwamba nimetiwa muhuri na Roho Mtakatifu, jinsi ninavyoishi, ninavyozungumza, na kutembea.”

²⁰¹ Tupe sauti kwenye piano, *Nampenda*. Mnalimaanisha kweli? Semeni, “Amina,” kama mnalimaanisha. Kweli mnapenda kujielezea huku kwa Yesu tunapouimba pamoja? Sote pamoja, kwa njia ya mtindo wa kale sasa, “Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza.” Sote pamoja sasa, hebu twende:

Nampenda, nampenda
 Kwani . . . mimi
 Na kununua wokovu wangu
 Juu . . . (Ni wengi sana hata siwezi
 kuwagusa.) . . . Kalvari . . . (Yule
 mwanamke . . . ? . . .)

²⁰² Hebu kidogo, katika kujituliza, endeleeni tu na utangulizi. Shetani alikuwa amemkatiza maskini mwanamke huyo, akamtorosha kutoka jengoni, Roho Mtakatifu akamshika huko nje na kumrudisha. Yuko mkutanoni sasa, ametulia. “Kwa Jina Langu watatoa pepo.” Nguvu ziko katika utamu na unyenyekevu, hilo ndilo linalofanya mambo kuwa makubwa kwa sababu ni unyenyekevu na utamu.

²⁰³ Hivi hamumpendi? Sasa, sote pamoja tena huku macho yetu yamefumbwa na mikono yetu imeinuliwa kuelekea Mbinguni, moyo wako wote:

Nampenda, na- . . . (. . . ? . . .) 

62-0127 Mtu Katili Kuliko Wote Nimjuaye
Ramada Inn
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org